AGENCY FOR PEACEBUILDING

KUJENGA AMANI program
building the peace together



# UCHAMBUZI WA MIGOGORO KATIKA MAENEO YA PWANI YA KENYA NA TANZANIA

## Taarifa ya utafiti

Disemba 2023

Co-funded by the European Union

## KUHUSU SHIRIKA LA AGENCY FOR PEACEBUILDING

Agency for Peacebuilding (AP) ni Shirika lisilo la kifaida lenye lengo la kustawisha hali na kusaidia katika utatuzi wa migogoro, kupunguza vurugu na kuchangia katika kuleta amani ya kudumu barani Ulaya, maeneo jirani na Ulaya na duniani kwa jumla. AP ni shirika la kwanza na Kitaliana linalojikita katika ujenzi wa amani. Hii inaifanya kuwa na nafasi ya kipekee katika bara la Ulaya: ambpo kwa upande mmoja linatafsiri na kuunganisha maudhui husika kwa ajili ya mashirika na taasisi za nchini Italia zinazofanyia kazi masuala ya amani na usalama; na kwa upande mwengine linaonesha uzoefu, uwezo na nyenzo makhsusi kwa ajili ya mfumo wa Italia, ambavyo vinaweza kusaidia katika kutatua migogoro.

## SHUKRANI

Timu iliyoshiriki katika uchambuzi wa migogoro inajumuisha Bernardo Monzani, Hashim Pondeza, Mikhail Silvestro Sustersic na Bernardo Venturi. Timu hii inapenda kutoa shukrani zake kwa taasisi za CEFA Onlus na WeWorld, ambao mchango wao ulikuwa ni muhimu sana katika kuhakikisha utafiti huu unakamlika kwa mafanikio. Aidha timu inawashukuru washirika wenyeji ambao mchango wao ulikuwa mkubwa sana katika kuendesha mahojiano ambao ni GRCF, MWARP, Samba Sports na Muleide. Msaada na muongozo wao ulikuwa wa thamani kubwa katika kuhakikisha ubora wa ukusanyaji wa taarifa. Mwisho, shukrani zetu ziende kwa wote ambao wameshiriki katika mahojiano na katika utafiti, kwa kutoa maoni yao muhimu katika uchambuzi wa migogoro.

Maoni yote yaliyomo katika ripoti hii ni ya waandishi, na kwa namna yoyote ile hayaakisi maoni ya CEFA au yoyote miongoni mwa washirika wake.

Taarifa hii imechapishwa kwa msaada wa kifedha kutoka Jumuiya ya Ulaya kupitia mradi wa “Kujenga amani - Building peace on the Swahili Coast”. Maudhui ya taarifa hii ni miliki ya kipekee ya shirika la Agency for Peacebuilding (AP) na kwa namna yoyote ile hayatachukuliwa kuwa ni msimamo wa Umoja wa Ulaya.

Co-funded by the European Union

www.peaceagency.org

*Picha ya nje kwa hisani ya CEFA Onlus (2023).*

**KWA KUSHIRIKIANA NA:**

CEFA
The seed of solidarity

We World

MWARP
MUSLIMS WOMEN ADVANCEMENT OF RIGHTS AND PROTECTION

SambaSports Youth Agenda
Talent-Education-Discipline

MULEIDE
DESENVOLVIMENTO

The Global Religions for Children Foundation
"Together for Children"

# YALIYOMO

UFUPISHO WA MANENO 5
MUHTASARI 6
HISTORIA YA MRADI 9
MBINU ZA UTAFITI 10
UCHAMBUZI WA MIGOGORO: KENYA 12
KWALE 14
MOMBASA 25
NAFASI YA UTAMADUNI WA WASWAHILI NCHINI KENYA 33
TANZANIA 36
MTWARA 38
TANGA 46
NAFASI YA UTAMADUNI WA WASWAHILI NCHINI TANZANIA 54
MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO 56

# UFUPISHO WA MANENO

| | |
|---|---|
| **AP** | Agency for Peacebuilding |
| **CAP** | County Action Plan/ Mpango Kazi wa Kaunti |
| **CSO** | Civil Society Organization/ asasi ya kiraia |
| **EU** | European Union/ Umoja wa Ulaya |
| **FGD** | Focus Group Discussion/ Majadiliano ya Kikundi Lengwa |
| **FGM** | Female Genital Mutilation/ Ukeketaji Wanawake |
| **GBV** | Gender-Based Violence/ Udhalilishaji wa kijinsia |
| **ISIS** | Islamic State in Syria/ Dola la Kiislamu nchini Syria |
| **KII** | Key Informant Interview/ Mahojiano muhimu ya watoa habari |
| **NAP** | National Action Plan/ Kazi wa Kwanza wa Kitaifa |
| **NSCVE** | National Strategy on CVE/ Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Vurugu za Misimamo Mikali |
| **P/CVE** | Prevention/ Countering of Violent Extremism/ Kuzuia/ Kukabiliana na Unyanyasaji wa Misimamo mikali |
| **PWD** | People with Disabilities/ Watu wenye ulemavu |
| **STI** | Science, Technology and Innovation/ Sayansi, teknolojia, uvumbuzi |
| **UN** | United Nations/ Umoja wa Mataifa |
| **WPS** | Women, Peace and Security/ Wanawake, Amani na Usalama |
| **YPS** | Youth, Peace and Security/ Vijana, Amani na Usalama |

# MUHTASARI

"Kujenga Amani: Building peace on the Swahili Coast (Kujenga amani katika mwambao wa Waswahili) ni mradi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) na kutekelezwa na shirikisho la taasisi za kiraia likiongozwa na CEFA Onlus. Mradi huu unadhamiria kuona nafasi iliyoimarika kwa mitandao ya vijana na taasisi za ngazi ya chini katika kushajiisha vijana wa maeneo ya mwambao yaliyochaguliwa nchini Kenya, Msumbiji na Tanzania, ili waweze kuwa mabalozi wa mabadiliko chanya katika jamii zao. Mradi huu unaendeshwa na dhana ya kuongozwa na jamii, dhana inayotambua kuwa jitihada zinazofanywa na taasisi za ngazi ya chini ni muhimu sana katika kuhakikisha amani ya kudumu na inayoamini katika kuwawezesha mtu mmojammoja, familia na wanajamii kuwa ni wadau katika jitihada za kujenga amani. Lengo la ujumla la mradi huu ni kuwa na vijana wa kike na kiume katika maeneo ya mradi yaliyochaguliwa wanaojitambua na wenye hamasa ya kujenga amani na kuleta mabadiliko chanya. Lengo makhsusi ni kwa mitandao ya vijana na taasisi rasmi na zisizo rasmi kushiriki katika kusambaza mafunzo ya ujenzi wa amani, kuepusha migogoro na kushajiisha ushirikishwaji.

Uchambuzi wa migogoro ulifanywa kwa ajili ya kutathmini migogoro na mienendo ya ujenzi wa amani katika maeneo yaliyochaguliwa ya mradi ambayo ni Kwale na Mombasa kwa upande wa Kenya na Mtwara na Tanga kwa upande wa Tanzania. Kipekee, uchambuzi ulilenga katika kutambua vikwazo na sababu zinazokwamisha mtangamano wa kijamii, hasa zile zinazoathiri haki na ushiriki wa vijana wa kike na kiume na kukwamisha ukuwaji wa maendeleo yao kama watu. Kwa kuongezea, uchambuzi ulijielekeza katika kutambua maeneo ya kuanzia na fursa za kujenga amani katika kila eneo. Shughuli za utafiti zilijumuisha mapitio ya kina ya nyaraka mbalimbali, mahojiano na wadau 33, na utafiti wa kimaelezo kwa jumla ya wadau 321 walio chini ya umri wa miaka 35.

Wakati wa zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa, mambo mengi muhimu yanayohusiana na amani na migogoro yalijitokeza katika maeneo yote ya mradi, nchini Kenya na Tanzania.

Mifano ya udhalilishaji wa kijinsia (GBV) na udhalilishaji wa majumbani ulioneakana kutapakaa na kuonekana kuwa jambo la kawaida kwa kiwango cha kutisha. Mifano hii ndiyo iliyoelezwa mara nyingi zaidi na wahojiwa wa jinsia zote. Licha ya hivyo, ni nadra kwa makosa ya aina hii ya udhalilishaji kuripotiwa na kuhukumiwa na uwajibakaji kwa wahusika ni wa kiwango kidogo sana. Udhalilishaji wa kijinsia na ule wa majumbani bado unaonekana kuwa ni unyanyapaa na waathirika wanasita kutafuta msaada na si aghalabu kuripoti polisi. Aidha, katika mazingira ambayo sheria na matendo kuhusiana na ndoa, talaka, mirathi na ardhi zinapendelea wanaume dhidi ya wanawake, migogoro ya majumbani ndio hali inayojitokeza mara nyingi ambapo usuluhishi na mbinu za utatuzi wa migogoro zinahitajika zaidi.

Wahojiwa wengi wanadhani kuwa makundi ya kihalifu ya vijana ndio tishio kubwa la amani. Wafuasi vijana wa makundi hayo mara nyingi huwa ni vijana wadogo chini ya miaka 18, waliotoroka shule ya msingi au wasio na ajira, mayatima au waliolelewa na mzazi mmoja, au watoto waliokulia katika mazingira ya umasikini wanaojaribu kusaidia familia zao. Katika maeneo kama ya Mombasa, vijana hawa wamekuwa ni kundi muhimu sana kwa wasambazaji wa madawa ya kulevya. Aidha, makundi ya vijana yamekuwa yakitumika na wanasiasa katika mikakati yao ya kuwania madaraka na baadhi ya wakati hutumika katika kutishia wapinzani na kuonesha hasira zao katika mikutano ya hadhara.

Umasikini na ukosefu wa ajira ni sababu kuu zinazowasukuma vijana kujiunga na makundi ya kihalifu. Zaidi ya hivyo, vijana wasio na ajira, wavivu na masikini kipekee wapo katika hatari ya utumiaji wa madawa ya kulevya. Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya utumiaji wa madawa ya kulevya na uhalifu, hasa kupitia uhalifu wa makundi. Wahojiwa wengi wamethibitisha kuwa matumizi ya madawa ya kulevya huwasukuma vijana waraibu kutumia nguvu na kufanya uhalifu. Watumiaji wa madawa mara nyingi hutenda uhalifu ili kupata fedha ya kununua madawa, na wanachama wa makundi mengi huwa wanaendeshwa na nguvu ya madawa wakati wanapofanya uhalifu.

Migogoro kati ya rika tofauti na mitazamo hasi ya jamii dhidi ya vijana pia ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyojitokeza katika maeneo yote ya mradi. Vijana wameonekana na wahojiwa wengi kuwa ni kitovu cha uhalifu na tishio kubwa la usalama. Aidha, vijana mara nyingi wanaelezwa na wazee kuwa wapo katika hali ya mchanganyiko wa uvivu, kukata tamaa na kukosa utayari wa kujipatia kipato kwa uaminifu na bidii ya kazi. Tayari kumekuwepo na mikinzano, siyo tu baina ya vijana na jamii, lakini pia, na zaidi, kati ya vijana na vyombo vya usalama, ambavyo vinatuhumiwa na vijana kwa kuchukua hatua nzito za kiusalama na matumizi makubwa na mabaya ya nguvu. Miongoni mwa vijana kuna hisia ya kutengwa na kutokuwa na matumaini hasa kwa wale wasio na elimu wala ujuzi wowote wa kazi. Hata hivyo, wakati vijana wapo katika hatari ya matumizi ya nguvu na kufanya uhalifu, bado wanaonekana kuelemewa na hali ya kutokuwa na usalama wa kijamii na kiuchumi pamoja na kutengwa, na mara nyingi wao wenyewe huwa ni wahanga wa unyanyasaji wa majumbani, fujo za kisiasa na uovu. Pamoja na yote haya, mzigo wanaokabiliana nao vijana hawa hauchukuliwi kwa uzito wake, na badala yake kinachoangaliwa ni jinsi gani vijana hawa ni hatari kwa jamii.

Kwa muktadha huo, jitihada za ujenzi wa amani zinapaswa kufanya kazi katika kubadili mitazamo ya wazee dhidi ya vijana. Kwa hakika, mitazamo hii ya upande mmoja inasababisha uzito zaidi katika kuwashirikisha vijana walio katika mazingira hatarishi, kuanzisha majadiliano ya rika tofauti na kuwafanya vijana kuwa na mchango chanya kwa jamii zao.

Kwa sasa vijana wamekuwa wakishirikishwa kwa kiasi kidogo sana katika mipango mbalimbali ya ujenzi wa amani, kuimarisha usalama na utatuzi wa migogoro. Vijana hawa, siyo tu kwamba ni wadau muhimu kwa amani, lakni ni wachangiaji wazuri wa mabadiliko pale wanaposhirikishwa. Hata hivyo, kumekuwa na uenezaji wa kiwango cha chini sana wa mchango wa vijana katika amani na usalama. Jitihada kubwa zinazofanywa na vijana zinabaki kuwa zinafifilizwa na kukosa kuonekana au kupata msaada wa kifedha na kitaalamu. Zaidi ya hayo, kuna itikadi zinazokandamiza ushiriki wa vijana; kwamba kiutamaduni vijana wanaonekana kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi na mara nyingi wanadharauliwa kwa sababu watu wazima na wazee wanaamini kuwa wao pekee ndio wanajua kila kitu. Ushirikishwaji wa vijana wa kike ndio upo katika hali mbaya zaidi.

Kwa kumalizia, utamaduni wa Kiswahili kwa hakika ni njia inayowaunganisha watu kwa kuwaleta pamoja na kushinda mipaka yao ya kijamii kwa kutumia lugha na kuchochewa na ukarimu na maisha ya umoja. Mikusanyiko na sherehe inachukuliwa kuwa ni matukio muhimu ya kuwaleta wanajamii pamoja na kuwa ni maeneo sahihi ya kujadiliana na kubadilishana mawazo. Pamoja na kwamba utamaduni wa Kiswahili unaonekana na baadhi ya watu kuwa unapitwa na wakati, wahojiwa wengi wa utafiti huu wanaamini kuwa utamaduni huu unapaswa kudumishwa na kuenziwa.

Yafuatayo ni mapendekezo yaliyokusanywa kutokana na uchambuzi wa migogoro:

- Umuhimu wa kuyaunganisha makundi lengwa ya vijana (yale yanayojihusisha na uhalifu, uraibu, na wasio na ajira) na wadau muhimu (taasisi, wazee, viongozi wa dini, polisi na maafisa usalama)
- Kuhakikisha jitihada zinazoendeshwa na jamii kwa kutumia sera na mifumo iliyopo.
- Kutengeneza mazingira salama na shirikishi.
- Kujenga uwezo katika maudhui ya amani na usalama pamoja na kutoa mafunzo ya kiufundi na vitendo (TVET).
- Kuimarisha maelewano na majadiliano kati ya rika tofauti.
- Kuhakikisha ushirikishwaji mkubwa wa vijana na kuhamasisha elimu rika.
- Kukabiliana na pengo la kuwaponya vijana na udhibiti wa vijana katika matumizi ya madawa.
- Daima kuwa makini na hali tete ya migogoro.

# HISTORIA YA MRADI

“Kujenga Amani: Building peace on the Swahili Coast (Kujenga amani katika mwambao wa Waswahili) ni mradi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) na kutekelezwa na shirikisho la taasisi za kiraia likiongozwa na CEFA Onlus. Mradi huu unadhamiria kuona nafasi iliyoimarika kwa mitandao ya vijana na taasisi za ngazi ya chini katika kushajiisha vijana wa maeneo ya mwambao yaliyochaguliwa nchini Kenya, Msumbiji na Tanzania, ili waweze kuwa mabalozi wa mabadiliko chanya katika jamii zao. Mradi huu unaendeshwa na dhana ya kuongozwa na jamii, dhana inayotambua kuwa jitihada zinazofanywa na taasisi za ngazi ya chini ni muhimu sana katika kuhakikisha amani ya kudumu na inayoamini katika kuwawezesha mtu mmojammoja, familia na wanajamii kuwa ni wadau katika jitihada za kujenga amani.

Mradi huu unakusudia kusaidia kutengeneza fursa mpya kwa vijana wa kike na wa kiume kuwawezesha kushiriki katika majadiliano na wanajamii na wafanya maamuzi katika masuala ya usalama, kuepusha migogoro na usawa wa kijinsia. Sambamba na hayo, mradi unaweka mkazo katika kutambua vipengele muhimu vya utamaduni wa Kiswahili vinavyojifungamanisha na amani na katika kuendeleza vipengele hivyo ili kuepusha na kupunguza utokeaji wa migogoro na hatimae kuhuisha mafungamano na mshikamano wa jamii. Sanaa shirikishi, shughuli za kitamaduni na michezo zinawaleta pamoja wanajamii, wasanii na wanaharakati wa masuala ya amani ili kutengeneza utamaduni mpya unaofurahia amani, usawa wa kijinsia ma mshikamano wa jamii.

Lengo la ujumla la mradi huu ni kuwa na vijana wa kike na kiume katika maeneo ya mradi yaliyochaguliwa wanaojitambua na wenye hamasa ya kujenga amani na kuleta mabadiliko chanya. Lengo makhsusi ni kwa mitandao ya vijana na taasisi rasmi na zisizo rasmi kushiriki katika kueneza mafunzo ya kujenga amani, kuepusha migogoro na kushajiisha ushirikishwaji.

Mradi huu umegawanyika katika maeneo manne makuu:

- Kuongeza elimu na uelewa kwa taasisi za kiraia zilizo ngazi ya chini pamoja na vijana ili kuchangia kikamilifu katika kujenga jamii yenye amani;
- Kuimarisha uwezo wa vijana kuwa mabalozi wa mabadiliko chanya katika jamii zao;
- Kujenga amani kwa vitendo kwa kutengeneza fursa mpya za majadiliano zinazoendeshwa na jamii na zinazochangia katika amani; na
- Kufurahia na kutetea uwepo wa amani, usawa wa kijinsia na mtangamano wa kijamii.

# MBINU ZA UTAFITI

Lengo kuu la uchambuzi wa mradi wa "Kujenga Amani" ni kutathmini mienendo ya migogoro na ujenzi wa amani katika maeneo yaliyochaguliwa na mradi ambayo ni Kwale na Mombasa kwa upande wa Kenya; na Mtwara na Tanga kwa upande wa Tanzania. Kipekee, uchambuzi unalenga katika kubainisha vikwazo na sababu zinazokwamisha au kuzorotesha mfugamano wa kijamii, hasa zile zinazoathiri haki na ushiriki wa vijana wa kike na kiume na kukwamisha ukuwaji wa maendeleo yao kama watu. Kwa kuongezea, uchambuzi ulijielekeza katika kutambua maeneo ya kuanzia na fursa za kujenga amani katika kila eneo.

Mbinu za uchambuzi ni linganishi na zimejikita katika mfumo wa mbinu mchanganyiko. Kimsingi, zoezi la ukusanyaji taarifa lilifanyika kwa njia ya maelezo lakini pia lilihusisha taarifa za kitakwimu. Mradi umejielekeza katika kutumia mbinu ya uwezeshaji ambayo inalenga katika kuipa nguvu ujuzi usiothaminiwa, ukiwemo ule unaomilikiwa na makundi yaliyotengwa. Muhimu ni kuwa mbinu ya utafiti imewekwa katika kutambua mienendo katika ngazi ya kaunti na kaunti ndogo ndogo. Mbinu hii imechaguliwa ili kuakisi lengo kuu la mradi, ambalo ni kuhamasisha mabadiliko katika ngazi ya chini, na pia kwa kutambua ukweli kwamba uchambuzi katika ngazi hii hauthaminiwi au hauonekani kabisa katika uchambuzi wa migogoro. Hata hivyo, mbinu hii ya uwezeshaji imetumika kwa kiwango kidogo sana, hivyo mengi zaidi yanaweza kufanywa kwa mbinu hii katika tafiti zitakazofuata.

Shughuli za mradi zilijumuisha uhakiki wa kina wa nyaraka mbalimbali, mahojiano kadhaa na wadau husika pamoja na utafiti wa maelezo. Uhakiki wa nyaraka ulijumuisha nyaraka 100 ambazo zilihusisha nyaraka kuhusu chambuzi za migogoro zilizopita, tafiti mbalimbali na ripoti, tathmini za miradi, makala za kitaalamu, takwimu rasmi, na taarifa nyengine zisizothibitishwa *(grey literature)* zilizotolewa na wadau husika kama vile CSOs, na wadau wa usalama na amani katika nchi hizi. Orodha kamili inapatikana katika kiambatisho N.1. Mahojiano ya moja kwa moja na wadau yalihusisha wataalamu na wadau muhimu kutoka mamlaka za serikali za mitaa, vyombo vya sheria, taasisi za kiraia, wanajamii wa maeneo husika (wakiwemo viongozi wa dini na wazee). Jumla ya mahojiano 33 yalifanyika, 16 Kenya (9 Kwale na 7 Mombasa) na 17 Tanzania (10 Mtwara na 7 Tanga). Mwisho, utafiti ulifanyika katika maeneo yote ukijumuisha wahojiwa 321 walio chini ya umri wa miaka 35, ambapo kwa upande wa Kenya yalikuwa 143 (66 Mombasa na 77 Kwale) na 178 kwa upande wa Tanzania (80 Mtwara 98 Tanga). Jumla ya wahojiwa wanawake katika utafiti huu ilikuwa ni 161, wakati kwa upande wa wanaume ilikuwa 160. Utafiti ulijipatia taarifa kutokana na maswali yaliyoandaliwa kwa mujibu wa viashiria vya mradi, na uliruhusu uchambuzi wa taarifa kwa mujibu wa eneo, jinsia na hali ya kuwa au kutokuwa na ajira.

Kiujumla, hakukuwa na changamoto kubwa wakati wa kufanya utafiti huu. Mapungufu pekee labda yanaweza kuonekana katika ubora wa taarifa zilizokusanywa ambao umetoa taarifa za kiujumla kuhusiana na mienenendo ya migogoro, lakini ukashindwa kutoa taarifa za ndani zaidi kuhusiana na vipengele mbalimbali vya migogoro vilivyobainishwa. Kwa mfano, wakati utafiti huu umeweza kuonesha unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa jinai kama mienendo muhimu, na kuunganisha mienendo hiyo na mitazamo ya kutokuwepo kwa haki na changamoto za kiuchumi, utafiti hakuweza kwenda mbali zaidi kuonesha nguvu inayowasukuma vijana kuamua kujiunga na makundi ya kihalifu. Katika hali hii, uchambuzi huu wa migogoro unapaswa kuchukuliwa kama ni hatua moja inayotoa muongozo kwa maeneo mengine ya kufanyiwa utafiti hapo baadae.




*Vijana wa Kikenya wakishiriki katika mashindano ya michezo (Picha kwa hisani ya Samba Sports Youth Agenda, 2020).*

# UCHAMBUZI WA MIGOGORO: KENYA

Kenya, nchi inayochukuliwa kama sehemu yenye amani, utulivu na demokrasia katika ukanda uliogubikwa na hali tete ya kisiasa, inaonesha kiuhalisia hali tofauti inayoambatana na migogoro ya ndani. Kama taarifa nyingi zinavyoonesha, nchi ya Kennya inapambana na migogoro ya kijamii iliyoota mizizi ambayo inaonekana kuongezeka[1] maradufu. Matukio ya vurugu na fujo mara nyingi yanadhihirisha hisia za malalamiko ya kijamii na kihistoria ya jamii za watu wa Kenya ambayo yametokana na utawala kikoloni wa Kiengereza na kuendelea kwa vizazi na vizazi. Kwa sasa, changamoto kubwa inayoelezwa kuikumba Kenya kama taifa ni pamoja na mgawanyo usio sawa wa rasilimali, kukosekana kwa usawa katika jamii, umasikini wa kupindukia, kiwango kikubwa cha uhalifu na tishio lililopo la vurugu na misimamo mikali. Kuwepo kwa tofauti za kiuchumi na kijamii au kutengwa kwa baadhi ya makundi ya watu kumeelezewa na wachambuzi wengi kuwa ndio kichocheo kikubwa cha aina mbalimbali za vurugu.

Katika kukabilina na changamoto hizi, Serikali ya Kenya imechukuwa hatua mbalimbali za kisheria, kisera na kimfumo ili kukabiliana na matatizo ya kimaendeleo, amani na usalama[2]. Kuanzishwa kwa mifumo ya kujenga amani, ikiwemo kamati za amani katika kaunti zote za Kenya, kunaakisi jinsi gani Serikali imejidhatiti katika kuondosha migogoro, jambo ambalo linaonekana pia katika kutungwa kwa Sheria na Sera mbalimbali. Miongoni mwa hizo ni Dira ya Kenya 2030[3], ambayo inadhamiria kuibadilisha Kenya kuwa nchi ya viwanda yenye uchumi wa kati, yenye uwezo wa kutoa maisha mazuri kwa wananchi wake wote ifikapo mwaka 2030 katika mazingira safi na salama.
Dira hii yenye maono ya muda mrefu inajielekeza katika utulivu wa kiuchumi, utawala na marekebisho ya sheria za ardhi, usawa na ugawanaji wa rasilimali, sayansi, teknolojia, uvumbuzi (STI) na usalama.

Kipekee katika masuala ya amani na usalama, Kenya imeanzisha mipango kazi miwili ya kitaifa kwa ajili ya kuendesha Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama[4], ambapo mpango wa kwanza ukitekelezwa katika kipindi cha 2016-2018, na wa pili katika kipindi cha 2020-2024. Mipango kazi hii ya Kitaifa imejielekeza katika kukabiliana na changamoto za unyanyasaji wa kijinsia, kushajiisha usawa wa kijinsia na kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake katika masuala yote yanayohusu amani na usalama.

Katika kipindi cha karibuni Kenya imejitahidi pia katika ushirikishwaji wa vijana, ambao ni kundi muhimu sana kidemografia nchini Kenya, ambapo takriban asilimia 80% ya watu wote wapo katika

[1] Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), “Rapid Conflict Assessment-Mombasa Count”y, 2021, p. 1.
[2] UN Women, “Report on Final Evaluation, Integrating Gender into Peace Support Operations in Eastern Africa”, May 2019, p. 4.
[3] Government of Kenya, “Kenya Vision 2030”, 2008.
[4] UNDP, “Kenya Launches Second National Action Plan on Women, Peace and Security”, May 2020.

umri wa miaka 35. Jitihada za Serikali zimetambua umuhimu wa kuwashirikisha vijana katika mikakati ya kijamii ya kujenga amani na kudumisha usalama[5], ambapo Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Kenya[6] ya mwaka 2019 imeweka vipengele muhimu vya vijana, amani na usalama, ikitambua kwamba amani ya kudumu na maendeleo endelevu vinaweza kupatikana tu kwa kupitia ushirikishwaji wa vijana, na kutatua kwa umakini changamoto zinazowakabili vijana.

Mwisho, ni muhimu kuzingatia umuhimu wa suala la vurugu za misimamo mikali katika kuandaa sera na mikakati ya kukabiliana na hali ya kutoweka kwa amani. Kenya inaendelea kushuhudia mashambulizi ya kigaidi, hasa katika mipaka yake na Somalia yanayoendeshwa na kundi la kigaidi la Al-Shabaab. Kwa upande wa masuala ya usalama, moja kati ya sheria muhimu ni Sheria ya Kuzuia Ugaidi iliyorekebishwa mwaka 2014 ambayo inaelezea hatua za kupinga ugaidi, upelelezi, na hukumu za matendo ya kigaidi. Kufuatia sheria hii, mwaka 2016 Serikali ya Kenya iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Vurugu za Misimamo Mikali[7] (NSCVE), mpango maalum wa kukabiliana na vyanzo vya vurugu za misimamo mikali, na kuzuia uingizaji wa watu katika itikadi za misimamo mikali. Kwa kuzingatia mbinu za kimkakati, ushirikishwaji wa jamii na mashirikiano na wadau mbalimbali, NSCVE inalenga katika kujenga uhimilivu dhidi ya nadharia za kimisimamo mikali na kujenga jamii yenye amani na yenye utulivu zaidi na, muhimu zaidi, ni kuwa mkakati wa NSCVE umesaidia kuibua mikakati mingine kadhaa ya kitaifa.




*Wanaharakati wanawake na wawakilishi wa taasisi za kiraia wakishiriki katika majadiliano yaliyoandaliwa na MWARP, Kenya (Picha kwa hisani ya MWARP, 2023).*


[5] National Crime Research Centre, Crime and Violence Prevention Training (CVPT), "Kwale and Bungoma County Crime and Violence Surveys", 2016, p. 4.
[6] Kenyan Ministry of ICT, Innovation and Youth Affairs, "Kenya Youth Development Policy 2019", November 2019.
[7] UN Women, "Civil Society's Voices on Violent Extremism and Counter-Terrorism Responses: Regional Perspectives from Eastern and Southern Africa", 2020, p. 9.

# KWALE

## Aina za migogoro na miundo ya vurugu

Kwale ni kaunti inayoonekana kwa kiasi fulani kuwa iko salama, ambapo migogoro pekee inayojitokeza inahusishwa zaidi na vitendo vya makundi ya kihalifu ya vijana na unyanyasaji wa majumbani. Umasikini na ukosefu wa ajira vinachukuliwa kuwa ndio sababu kuu za matatizo haya. Ukosefu wa ajira kwa vijana ni mkubwa sana na vijana wengi huacha shule wakiwa katika umri mdogo sana. Hivyo, kujiunga na makundi ya kihalifu, inaonekana, kwa vijana wengi kuwa ndio njia pekee ya kujipatia kipato. Ukweli kwamba wanachama wengi wa makundi ya kihalifu ni vijana kunachangia kusababisha mtazamo hasi kwa jamii dhidi ya vijana wote.

**Jadweli 1. Watu waliosema kuwa wanajisikia salama kutembea kurudi nyumbani katika kaunti ya Kwale.**




Kwale inahesabika kuwa ni miongoni mwa kaunti ambazo kihistoria zimekuwa zikikabiliana na tatizo la kutengwa kijamii na kiuchumi. Hadi leo hii, bado kaunti hii ina kiwango cha chini kabisa cha viashiria vya maendeleo ya binaadamu nchini Kenya[8], ambapo umasikini na ukosefu wa ajira upo katika kiwango cha juu sana[9]. Hali hii inatokea licha ya kuwa kwake na rasilimali kadhaa, ambazo kwa upande mwengine zinaweza pia kuwa ni chanzo cha migogoro. Kwa mfano, uchimbaji katika hifadhi ya madini ya titanium[10] iliyopo katika kaunti ya Kwale, kwa mujibu wa wachambuzi wengi, unahatarisha kuongezeka kwa hali tete au kusababisha migogoro mipya kuhusiana na udhibiti na faida zinazotokana na rasilimali hiyo[11]. Kwa upande wa elimu, Kwale inaonekana kuwa iko nyuma

[8] UN Kenya, "Leave No One Behind: Peace and Conflict Analysis", March 2022, p. 13.
[9] National Crime Research Centre, Crime and Violence Prevention Training (CVPT), "Kwale and Bungoma County Crime and Violence Surveys", 2016.
[10] Plan International, "Kenya Summary Report: Rapid Gender and Needs Analysis In Kwale", November 2022, p. 11 and p. 15.
[11] International Alert, "Going for Gold: Risks and Opportunities in Kenya's Extractives Sector", December 2021, p. 2.

zaidi ya sehemu yengine za Kenya, na kuacha shule hasa kwa vijana wa kike mara nyingi kunasababishwa na ndoa za kupangwa na uzazi wa mapema[12].

Kama ilivyoelezwa kabla, wahojiwa katika utafiti huu wameonesha kuwa Kwale kiujumla ni sehemu salama. Jadweli Nambari 1 hapo juu inaonesha kuwa miongoni mwa waliohojiwa, asilimia 79% ya wanawake na 75% ya wanaume wanajisikia wapo salama kutembea katika maeneo jirani, na asilimia 61% ya wanawake na 66% ya wanaume hawaoni kuwa ni hali ya kawaida kutokea matukio ya kihalifu katika maeneo wanayoishi. Wahojiwa wameonesha pia kuwa matukio yaliyozoeleka ya vurugu katika kaunti ya Kwale ni yale ya nyumbani, uhalifu na vurugu za kisiasa, ambapo wahojiwa wanawake wamekazia zaidi katika vurugu za majumbani huku wanaume wakizungumzia zaidi uhalifu wa kutumia nguvu.

Cha kuvutia ni kuwa mtazamo unaotokana na mahojiano unaonekana tofauti kidogo. Wengi miongoni mwa waliohojiwa wanadhani kuwa makundi ya kihalifu ya vijana ndio tishio kubwa la amani nchini Kenya. Kwa mujibu wa mwakilishi wa jumuiya moja ya kiraia, Kwale si sehemu salama kutokana na makundi ya kihalifu ya vijana, ambayo yanaonekana kuongezeka. “Matumizi mabaya ya madawa ya kulevya yapo kwa kiasi kikubwa, na wizi wa kutumia nguvu unaongezeka kutokana na matumizi ya madawa haramu”, alisema, huku akiongezea “wakati makundi ya [kihalifu] mtaani yanaposhambulia watu, wao hujiskia na furaha na kujihisi ni mashujaa[13]. Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, wanachama wengi wa makundi ya kihalifu ni vijana wa chini ya miaka 20 ambao wanatumia madawa ya kulevya hasa aina ya *Rohypnol*- ambayo wao huita *bugizi*- na wanaweza kushambulia mikusanyiko ya kijamii kama harusi, maziko au mechi za mpira wa miguu[14]. Kwa mujibu wa watoa taarifa wengi, matumizi ya madawa pia yanachochewa na sababu za kiuchumi kama vile ukosefu wa ajira, au uvivu unaotokana na kutokwenda shule. Wote wanakubaliana kuwa matumizi mabaya ya madawa yanawasukuma watu kufanya uhalifu na jinai[15].

Ukosefu wa ajira kwa vijana pia upo kwa kiwango kikubwa katika kaunti ya Kwale ambapo vijana wengi aidha hawana ajira au wana ajira isiyo rasmi ya kujishughulisha na biashara ndogondogo[16]. Aidha, kuna vijana wengi walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kipato kidogo cha familia na wategemezi wengi ndani ya kaya, ajira za utotoni, hali ya uyatima, mimba za mapema, kukosa motisha na msaada wa wazee[17]. Kwa sababu hiyo, [wachambuzi] wengi wanaliangalia suala la malezi kuwa ni kitu muhimu sana kilichokosekana Kwale.

[12]National Crime Research Centre, Crime and Violence Prevention Training (CVPT), “Kwale and Bungoma County Crime and Violence Surveys”, 2016.
[13] Interview with youth civil society leader, Kwale, August 2023.
[14] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[15] In interviews with religious leader and local government representative, Kwale, August 2023.
[16] James D., “Youth Unemployment and Security in Kenya: the Case of Kwale County (2010-2018”), February 2021, p. 58.
[17] UN Women, “From Where I Stand: Young people do care, and we have expectations of what we want in our communities and from our government”, November 2022; Otieno Airo M., Sika J. and Olendo C., “Determinants of Dropout and Transition Rates in Public Primary Schools in Kisumu East Sub-County, Kenya”, *Journal of Research Innovation and Implications in Education*, Vol. 6, Iss. 2, 2022, pp. 197 – 209.

Katika mazingira ambayo unyanyasaji wa kjinsia unaongezeka, jukumu la kulea na kuhudumia watoto linaonekana kuwa ndio sababu inayoongoza mikinzano katika majumba mengi[18]. Katika kila wanawake kumi ndani ya kaunti ya Kwale, saba kati yao ni wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia, hasa unyanyasaji wa majumbani na wa mirathi[19]. Wazazi mara nyingi huwa ni vijana wenye umri mdogo wanaojaribu kila hali kutengeneza maisha ya watoto wao. Aidha, kinachojulikana kuhusu wafuasi vijana wa makundi ya kihalifu ni kuwa wengi wao wanatoka katika familia zenye hali mbaya na mara nyingi huwa wamelelewa na mzazi mmoja kwa sababu baba au mama wanafanya kazi ughaibuni. Kwa mujibu wa kiongozi mmoja kijana katika Kaunti ya Kwale, "sehemu ya kuanzia ni wazazi: wamekata tamaa![20]. Kwale ni miongoni mwa maeneo yenye idadi kubwa ya wafanyakazi wanaotafuta ajira Mashariki ya Kati na Ghuba, ambapo wafanyakazi wa kike wa majumbani wanahitajika zaidi nchini Saudi Arabia. Hii ni kwa mujibu wa mwakilishi wa Shirika la Haki Afrika[21].

Licha ya suala hili kuwa sababu kuu inayopelekea migogoro na vurugu nchini Kenya, baadhi ya watu wanaamini kuwa viongozi wa dini, wazee na serikali kwa jumla bado hawajalichukulia suala hili kwa uzito unaostahiki. "Kuna hali ya kuchukulia mambo kikawaida tu miongoni mwa wadau husika", alieleza mwakilishi mmoja wa jumuiya ya kiraia, akiongeza kwamba kwa sasa hakuna sera inayoelekeza juu ya malezi; na kwa kuwa wengi kati ya vijana hawa ni wadogo, vyombo vya sheria vinakosa namna bora ya kuwashughulikia vijana hawa kisheria.

Vurugu zinazofanywa na vijana zinaathiri jamii nzima kwa ujumla. Misuguano kati ya makundi haya inapelekea pia kuchochea vurugu miongoni mwa watu wazima, kama inavyoelezwa na kiongozi mmoja wa jamii: "Vijana kutoka Waa hawawezi kuja Kitivo, na kinyume chake. Mgogoro umekuwa mkubwa kiasi cha kwamba wazazi taratibu wameanza kuwa maadui pia[22]. Hili linasababisha tatizo la kimtazamo: vijana wanaonekana na wahojiwa kuwa ni wakorofi na kwa ujumla wao wanabeba lawama kwa kile kinachofanywa na makundi maovu. Linapozungumzwa hili, baadhi hupingana nalo. Kiongozi mmoja wa kidini, kwa mfano, anaeleza kuwa katika kukabiliana na makundi ya vijana, yeye huwavuta na kuwafunza watu namna ya kuratibu vikundi vya ulinzi-jamii, maarufu kama sungusungu, ambavyo hufanya doria nyakati za usiku na kulinda maeneo jirani[23]. Sungusungu inachukuliwa kama vikosi mbadala vya ulinzi ambavyo jamii inaweza kuvitegemea.

---

Otieno G. C., "Socio-Economic Factors Influencing Students' Dropout Rates in Public Secondary Schools in Msambweni Sub County, Kwale County, Kenya", 2016.

[18] Search for Common Ground, "Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Kwale County", December 2020, p. 6.

[19] Zaka R. and Abdullahi H., Kenya News Agency (KNA), "Campaign Against Gender-Based Violence Kicks-Off In Kwale", November 2021.


[20] UN Women, "From Where I Stand: Young people do care, and we have expectations of what we want in our communities and from our government", November 2022.

[21] Onyango O., "Kilifi and Kwale lead in Middle East job seekers", The Star, October 2021.

[22] Interview with community elder in Kwale, August 2023.

[23] Interview with religious leader in Kwale, August, 2023.

**Jadweli 2. Watu waliosema kuwa vurugu za misimamo mikali ndio matokeo maarufu zaidi ya fujo**




Wakati makundi ya vijana yakionekana kuwa ni chanzo cha migogoro, vurugu zinazotokana na misimamo mikali hazionekani hivyo, ambapo utafiti umeonesha kuwa asilimia 11% tu ya wanawake na 13% ya wanaume waliielezea misimamo mikali kama aina maarufu ya migogoro. Jadweli nambari 2 hapo juu linaonesha taarifa zilivyochambuliwa kwa mujibu wa maeneo madogomadogo ndani ya kaunti ya Kwale na kwa mujibu wa umri wa wahojiwa. Kwa mfano, utafiti unaonesha tofauti kati ya mtazamo wa watu waliohojiwa wa Mwasembeni ambako kiwango cha walioona kuwa misimamo mikali ndio aina maarufu ya vurugu ni kikubwa tofauti na ile ya Lungalunga ambako kiwango kimeoneka kuwa ni kidogo sana. Kwa msingi huo, mahojiano yaliyofanyika yanaonesha kuwa watu katika kaunti hii angalau wanakubaliana kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya uhalifu na misimamo mikali. Ukosefu wa ajira, kwa mujibu wa watu wengi waliohojiwa, unapelekea kuwepo kwa mazalia mazuri ya watu kuingizwa katika misimamo mikali, na hivyo kupelekea vijana wengi kujiunga na makundi maovu na ya misimamo mikali ya kidini, kama ambavyo imeripotiwa na baadhi ya washiriki[24].

Hata hivyo, itikadi za misimamo mikali zimeibua majibu kutoka kwa serikali za mitaa. Mwaka 2017, kaunti ya Kwale ilibuni mpango wa hatua za kukabiliana na itikadi za misimamo mikali. Mpango huu ambao uliunganishwa na mpango wa Taifa wa NSCVE ulitoa muongozo kwa changamoto makhsusi zinazoikumba kaunti ya Kwale, na kuweka miongozo ya kuepusha au kukabiliana na vurugu za misimamo mikali nchini, katika namna zote mbili za kujikinga na mihemko ya vurugu na kurejesha amani[25]. Sehemu muhimu sana ya mpango huu ni namna ya utekelezaji wake unavyoendeshwa na

[24] James D., "Youth Unemployment and Security in Kenya: The Case of Kwale County (2010-2018)", February 2021, p. 56.
[25] Centre for Human Rights and Policy Studies (CHRIPS), "Workshop Note No. 2: Reviewing Kwale County's Action Plan on P/CVE", October 2020.

Jukwaa Shirikishi la Kwale la Kupinga Itikadi za Misimamo Mikali, mtandao unaowaleta pamoja wawakilishi wa serikali na taasisi za kiraia zinazofanyia kazi masuala ya kuepusha na kupamba na vurugu za misimamo mikali katika ngazi ya jamii[26]. Jukwaa hili linasaidia katika kuratibu na kuendesha mafunzo ya pamoja, kufanya mapitio na kuendesha mikutano ya kujitathmini[27]. Baadhi ya watu wanaliona jukwaa hili siyo tu kama mpango mzuri wa kuepusha migogoro, lakini pia kama chombo kinachoweza kuimarishwa zaidi kwa kuongeza ushirikishwaji[28].

## Viunganishi na vigawanishi

Viunganishi ni yale mambo yaliyopo, halisi au dhahania, yanayounganisha makundi yaliyo katika migogoro, wakati vigawanishi ni yale mambo yanayoyagawanya makundi yaliyo katika mgogoro na kufanya mgogoro kuwa mkali zaidi. Kwa mujibu wa wahojiwa wengi wanaume, michezo ni kiunganishi kikubwa katika kaunti ya Kwale. Michezo inachukuliwa kama ni nguvu ya kuwavuta watu[29] na yenye uwezo wa kuwaunganisha, na ambayo pia inaweza kutumika kama njia ya kuimarisha amani kwa kufanya kazi pamoja na vijana[30]. Mwakilishi wa serikali ya mtaa katika kaunti ya Kwale anakiri kwamba michezo ni njia endelevu ya kukabiliana na migogoro. "Michezo inaweza kuwakusanya vijana zaidi ya 3,000 kwa wakati mmoja", alisema, "na wanatumia rasilimali ndogo sana kwa [kuwakusanya] watu wenye asili mbalimbali"[31]. Mbali ya kuwaburudisha vijana, michezo pia ina nafasi ya kuwa daraja kati ya vijana na wanajamii wengine, wakiwemo wazee, viongozi wa dini, vyombo vya usalama na jamii kwa jumla[32]. Hata hivyo, ni lazima izingatiwe kuwa michezo inaweza kuwa na sura mbili: upande mmoja inaweza kuwa mikusanyiko ya kijamii yenye faida, na upande mwengine inaweza kuchochea vurugu pia. Kama anavyoeleza mwakilishi wa taasisi ya kiraia:

> *"Baadhi ya wakati timu iliyopoteza mchezo huanzisha mapigano na timu pinzani, maafisa wa michezo au hata wanajamii wa maeneo ya timu hiyo pale inapotokea timu moja kutokubaliana na maamuzi fulani kama vile penalti, kadi nyekundu, kukataliwa goli na kadhalika. Kwa upande mwengine, michezo inasaidia kuwahusisha vijana wavivu ambao mara nyingi huwa wanafikiria kujiunga na uhalifu. Kwenye michezo, vijana hao hujifunza kufuata taratibu, jinsi ya kutendeana wema na wengine, kuheshimiana na tabia hizi huwabadilisha vijana hawa taratibu kuwa vijana wazuri[33]".*

---

[26] Human Rights Agenda (HURIA), "Special Report: An Assessment of the First generation Kwale County Action Plan Preventing & Countering Violent Extremism", November 2020, p. v.
[27] Ibid., p. 9.
[28] Ibid., p. vii.
[29] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[30] Interview with civil society representative, Kwale, August 2023.
[31] Interview with local government representative, Kwale, August 2023.
[32] Interviews with religious leader and civil society representative, Kwale, August 2023.
[33] Interview with civil society representative, Kwale, August 2023.

Kitu kingine cha msingi kinachowaunganisha watu kwa mujibu wa watu waliohojiwa ni dini, kwa sababu "inawaleta wanajamii wote pamoja licha ya tofauti zao za kisiasa, rangi na maeneo wanayotokea[34]. Hili linathibitishwa na takwimu za utafiti ambapo asilimia 89% ya wanawake na 97% ya wanaume wameonesha imani yao kubwa kwa viongozi wa dini linapokuja suala la utatuzi wa migogoro miongoni mwa makundi ya jamii. Cha kuvutia zaidi ni kuwa vijana nao wana imani kama hiyo, ambapo asilimia 89% ya wahojiwa wenye miaka kati ya 18 na 24 wamekubaliana na maelezo kuwa ni jukumu la viongozi wa dini kutatua migogoro kati ya jamii moja na nyengine (idadi hasa ni asilimia 100% kwa wahojiwa kati ya miaka 25 – 29, na 95% kwa wahojiwa wa kati ya miaka 30 – 35). Matarajio haya yanapokewa na kukubaliwa na viongozi wa dini wenyewe pia. Kama alivyoeleza mmoja wao, "sisi kama viongozi wa dini huwa hatulali usiku: tumejaribu kuwafikia vijana kupitia shughuli za kijamii na kupitia majukwaa yetu kuhubiri amani na kufanya majadiliano na wao; imekuwa ni ajenda yetu daima kuzungumza nao. Tunahudhuria shughuli za kijamii kwa ajili ya kuleta amani[35].

Ripoti zilizopitiwa, pamoja na mahojiano na watoa taarifa zinaeleza kiasi gani mikutano isiyokuwa rasmi inaweza kuwa viunganishi muhimu. Mikutano ya baraza, kipekee, ni maeneo kwa ajili ya wazee wa jamii kupashana habari na kuamiliana hata na vijana[36]. Baraza ni neno la Kiswahili linalomaanisha mkutano wa wazi ambao hutumika kama jukwaa kwa ajili ya kueneza uelewa, kutoa majibu kwa changamoto zinazoikumba jamii fulani, kupashana taarifa muhimu, kutoa fursa kwa wananchi kueleza changamoto na kupendekeza njia za utatuzi. Baraza hutumika pia kama majukwaa ya kutolea taarifa kwa umma na kama njia ya haraka ya kukusanya maoni ya wananchi kutokana na changamoto fulani inayowasibu[37]. Sherehe za kijamii na kidini pia ni matukio muhimi yanayowafanya watu kuungana. Shughuli za harusi, kwa mfano, zinawaleta watu wanatoka katika jamii zinazohasimiana kusherehekea pamoja[38].

Katika muktadha huohuo, ingawa hii kwa namna rasmi kidogo, ni uwepo wa Jukwaa la Vijana wa Kwale, jukwaa la kijamii lisilo na mrengo wa kisiasa, lililoanzishwa na kuendeshwa na vijana, ambalo kwa mujibu wa watoa taarifa wengi ni sehemu inayowaleta vjana pamoja kupitia midahalo na ushauri nasaha[39] na pia kuendesha majadiliano ya kijinsia yanayowakutanisha akina mama na watoto, ambayo ni muhimu kwa ajili ya kukusanya maoni na mahitaji yao makhsusi[40]. Kiujumla, Asasi za Kiraia

[34] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[35] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[36] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[37] UN Uganda, "Human Rights Baraza: A Handbook on Conducting Community Public Meetings", April 2014.
[38] Interview with local government representative, Kwale, August 2023
[39] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[40] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.

(AZAKi) pia zinaonekana kuziunganisha jamii pamoja kupitia shughuli mbalimbali za kujenga uelewa na kuhamasisha, huku zikiwaleta watu pamoja[41].

Kigawanishi pekee kilichoelezewa mara nyingi ni makundi ya kihalifu ya vijana na uwezo mdogo unaoonekana wa kuyadhibiti makundi hayo. Kama ilivyoelezwa kabla, tatizo la makundi ya vijana linahusishwa pia na matumizi ya madawa ya kulevya, na si wazee wala mamlaka waanojua namna ya kulikabili suala hili. Hii ndio maana, kwa mujibu wa wahojiwa, kuna ugumu kwa jamii na jeshi la polisi kuchukua hatua dhidi ya makundi ya vijana[42].

Kigawanishi kingine muhimu ni siasa, na hasa harakati za kuwania madaraka na rasilimali miongoni mwa wanasiasa. Hili linaunganishwa kwa ukaribu na mtazamo hasi katika uwanja wa siasa, ambao watu wengi wanaamini kuwa hakuna uwazi na uwajibikaji, na ambako undugu unatumika vibaya. Siasa kiujumla haziathiri watu moja kwa moja katika maisha yao ya kila siku, lakini inaathiri jinsi watu na familia zinavyogombania mali, mirathi na ardhi[43]. Kama ilivyoelezwa hapo kabla, vurugu za kisiasa ndio matukio yanayotokea mara nyingi zaidi kwa mujibu wa asilimia 37% ya wanawake na asilimia 31% ya wanaume waliohojiwa.

| VIUNGANISHI | VIGAWANISHI |
|---|---|
| Michezo | Udhibiti wa changamoto za makundi ya vijana |
| Dini | Siasa/ kuwania madaraka na siasa |
| Sehemu za mijadala | Familia kugombania mirathi |
| Shughuli za asasi za kiraia | Undugu na ukabila |
| Sherehe | Upendeleo na ufisadi |

## Uchambuzi wa wadau na uhusika wao

Zoezi la uchambuzi wa wadau limefanyika kama sehemu ya uchambuzi wa migogoro ili kuainisha wahusika wakuu wanaochangia katika mienendo ya migogoro na amani katika kaunti ya Kwale. Sehemu hii inatoa maelezo kwa kila kundi la wahusika lililobanishwa, ikijumuisha taarifa zaidi kuhusiana na mitazamo na matendo yao kama ilivyoripotiwa.

[41] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[42] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[43] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.

## Mamlaka za Serikali

Wahojiwa muhimu wanathamini kazi inayofanywa na mamlaka za serikali ya kutatua au kukabiliana na vurugu na mivutano katika eneo la Kwale, na wanatambua mchango wa mamlaka hizo katika kuleta amani na maendeleo. "Uongozi wa kaunti ya Kwale na serikali ya kitaifa", ameeleza mwakilishi wa jumuiya ya kiraia ya vijana, "zimefungua milango hasa katika masuala ya amani[44]". Uendeshaji wa vikao vya baraza katika maskani za vijana, wazee na wanawake pia limeangaliwa kama jambo la kuthaminiwa sana kwa sababu lina matokeo chanya na huchangia katika kutatua migogoro ya ndani[45].

Hata hivyo, wajihi wa mamlaka za serikali unaangaliwa vibaya kutokana na mitazamo ya rushwa na upendeleo. Aidha, kuna hali ya hofu na kutoaminiana linapokuja suala la kuripoti uhalifu wa kikatili kwa polisi[46]. Kutokuchukuliwa kwa hatua madhubuti kwa wakati na vyombo vya usalama kunapelekea jamii kutokuwa na imani kwa vyombo hivyo, na hivyo kuchagua njia mbadala za kushughulikia matatizo yao, wakati mwingine kwa njia za vurugu (kama vile kudai haki kwa kutumia nguvu ya umma)[47]. Kwa msingi huo, watu hupendelea kwenda katika mahakama za kangaroo zinazoendeshwa na viongozi wa dini, wazee na wanajamii wanaoaminika badala ya kukimbilia katika mifumo ya serikali.

Imani kwa mamlaka za serikali ni suala linalotegemea mtu na mtu, ambapo heshima na uaminifu zaidi inaelekezwa kwa maafisa wanaotoka katika jamii husika au wanaofanya nao kazi kwa ukaribu, ambao hutembelea mitaa husika mara kwa mara. Watu hawa wanachukuliwa kama ni wenyeji au wapo karibu na changamoto za maeneo hayo[48], ilhali maafisa wa ngazi za juu za serikali wanaonekana kuwa ni mafisadi tu[49]. Waliohojiwa pia wameeleza kuwa mara nyingi fedha za maendeleo zinazotolewa na serikali zinagawanywa isivyo sawa na kwamba baadhi ya maafisa waandamizi hufanya upendeleo, na hivyo kusababisha hali ya taharuki na hasira miongoni mwa raia.

Wanasiasa wana nafasi kubwa nao katika migogoro. Wao "wanadhibiti hali ya amani na hali ya vurugu: wanaposema hakuna maandamano watu husikiliza na amani hutawala, lakini kwa upande mwengine wanaweza kuamuru maandamano katika nchi nzima"[50]. Kwa sababu hii, baadhi ya waliohojiwa wameeleza kuwa ushiriki mkubwa wa serikali ya kaunti na ile ya kitaifa, ikichanganywa na kuwepo kwa majadiliano ya wazi zaidi na vijana, kunaweza kuwa na athari kubwa nzuri[51].

[44] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[45] In interviews with religious leaders and with a local government representative, Kwale, August 2023.
[46] Interview with community elder, Kwale, August 2023.
[47] In interviews with religious leader and youth leader, Kwale, August 2023.
[48] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[49] Interview with civil society representative, Kwale, August 2023.
[50] Interview with religious leader, Kwale, August 2023.
[51] In interviews with local government representative and community elder, Kwale, August 2023.

## Asasi za kiraia (AZAKi)

Asasi za Kiraia ni muhimu sana katika masuala ya kujenga amani na usalama pamoja na upatanishi na utatuzi wa migogoro, kwa mujibu wa wahojiwa wote wakuu. Asasi za Kiraia wanaziwakilisha kikamilifu jamii zisizo na sauti kupitia vikao, majadiliano na shughuli za kitamaduni[52] na kujenga uelewa juu ya masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa watoto, uwezeshaji wa vijana, haki za wanawake, haki za kisheria katika mirathi na afya ya uzazi[53]. Pia wanajitolea katika kuwalea na kuwasaidia vijana pamoja na kujadiliana nao masuala ya usalama. Shughuli za AZAKi, kwa wastani, zina sifa ya kuwa shirikishi. Kwa mfano, mwakilishi mmoja wa taasisi ya kiraia alitaja jukwaa la michezo la Magnet, jukwaa la kienyeji ambalo kwa kawaida hufanyika katika maeneo ya nje kwa ajili ya kujenga uelewa kuhusu masuala ambayo yanaathiri jamii, huku ikishirikisha hadhira katika majadiliano ya kujenga na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zao[54]. Asasi za Kiraia mara nyingi ndizo ambazo hutoa elimu ya uraia, ambayo imesaidia kuzuia vurugu na taarifa potofu baada ya uchaguzi, kupunguza uhalifu na kujenga imani kubwa kwa jamii[55].

Katika mahojiano na watoa habari wakuu, asasi za kiraia zilizotajwa zaidi ni Samba Sports, ambayo ni mshirika wa mradi, Youth and Women for Peace and Sustainable Development (YOWPSUD), inayojikita katika ustahamilivu wa pamoja dhidi ya migogoro, shirika la Kiafrika la HAKI Africa na Muslims for Human Rights (MUHURI), ambayo inafanya kazi nzuri katika eneo lote la Pwani, na taasisi ya Human Development Agenda (HUDA), shirika la vijana linalofanya kazi Kwale kuangazia masuala ya kukinga vurugu za misimamo mikali, ulinzi wa watoto na haki za binadamu.

## Vijana

Katika Kaunti ya Kwale, vijana wameshiriki katika mipango mbalimbali ya amani, usalama na kutatua migogoro, ingawa kwa kiwango kidogo[56]. Mbali na miradi inayofadhiliwa na mashirika ya kimataifa (kama vile Search for Common Ground), kuna jitihada pia zinazofanywa na taasisi za ndani kama vile Baraza la Vijana la Kwale ambalo limetajwa kabla, linaloongozwa na vijana na linaloziwezesha jamii zilizotengwa kwa kuwapatia ufumbuzi endelevu; au taasisi ya Kwale Youth Governance and Consortium (KYGC), ambayo inafanya kazi katika kuhamasisha utawala bora na wa uwazi. Katika mipango hii, vijana wana fursa ya kuonesha uwezo wao wa kuleta mabadiliko na amani, na kuna ushahidi kwamba wanaweza kuwa na matokeo mazuri. Watu wote waliohusika katika utafiti huu wanaona shauku, kwa upande wa vijana wa kike na wa kiume, ya kuhusishwa zaidi, na wana imani kuwa ushirikishwaji mkubwa zaidi ungepelekea mshikamano mkubwa wa kijamii.

---

[52] In interviews with religious leader and youth leader, Kwale, August 2023.
[53] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[54] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.
[55] Interview with local level representative, Kwale, August 2023.
[56] Search for Common Ground, "Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Kwale County", December 2020.

Hata hivyo, juhudi nyingi za vijana bado zimefichwa na hazipati kuonekana kwa namna yoyote au kupata msaada wa kifedha na kiufundi[57]. Aidha, bado kuna vikwazo vinavyokwamisha ushiriki wa vijana. Waliohojiwa wanadai kuwa vijana mara nyingi huwa hawana utaalamu na ujuzi unaohitajika ambao ungewawezesha kushiriki kikamilifu na kwamba badala yake wanavutiwa zaidi na shughuli za kuzalisha kipato kuliko kushiriki katika mikutano ya kufanya maamuzi kama vile mabaraza. Kwa kuongezea, vijana mara nyingi hutafsiriwa na watu wazima kuwa wana mwelekeo uliochanganyika na uvivu, kiburi na kukata tamaa, hali inayowafanya wawe watazamaji na kutokuwa na hamu ya kufanya lolote. Muhimu zaidi, mtazamo hasi dhidi ya vijana hauonekani tu miongoni mwa watu wenye fikra za kihafidhina, kama vile viongozi wa kidini, lakini pia wawakilishi wengi wa asasi za kiraia.

Mtazamo walio nao wazee dhidi ya vijana, kama ilivyoelezwa na wahojiwa kadhaa, unastahili kuangaliwa kwa kina. Vijana wanachukua nafasi kubwa katika vita na uhalifu katika kaunti ya Kwale[58]: wao ni wahalifu ndio, lakini pia ni waathirika na wahusika wakubwa wa amani. Wakati vijana kwa hakika wako katika hatari ya kuleta vurugu na kufanya uhalifu, vijana haohao pia wanaonekana kuelemewa kupita kiasi na kukosa usalama wa kijamii na kiuchumi na mara nyingi wao wenyewe ni waathirika wa unyanyasaji wa majumbani, vurugu za kisiasa au uhalifu.

Licha ya hayo, matatizo yanayowakabili vijana mara nyingi hayatiliwi maanani, na badala yake mkazo mubwa unawekwa katika kuangalia hatari inayoletwa na vijana hao kwa jamii. Kwa mujibu wa kiongozi kijana wa jamii kutoka Kwale, wanaume wazee hawafahamu kwamba ili kuweza kuwashirikisha vijana katika maamuzi kuhusu amani na usalama, mtu anayeaminika na anayeweza kuamiliana na vijana lazima ashirikiane nao. Kwa maneno mengine, vijana lazima kuwashirikisha vijana wengine katika mchakato huu. Na kuna mifumo kama ile ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kenya ambao unapaswa kutumiwa na kuimarishwa zaidi ili kuwashirikisha vijana[59]. Aidha, vijana mara nyingi hukosa taarifa muhimu kuhusu kushiriki shughuli mbalimbali, kwa sababu taarifa hizo hutumwa kwa wale tu ambao tayari wamekuwa na uzoefu wa kushiriki au kwa kuhusika kwao na mtandao au jukwaa fulani[60]. Na kuna itikadi pia zinazozuia ushiriki wa vijana: "maoni na fikra za wachache wanaoshirikishwa hayachukuliwi kwa uzito; ni mwiko kuwasema wazee [ambao] maoni yao yanapewa kipaumbele zaidi kuliko yale ya vijana" alisema mwakilishi wa asasi za kiraia"[61]. Vijana wote wanafahamu upendeleo huu dhidi yao: kama kiongozi mmoja kijana wa jamii kutoka Kwale alivyosema, “kama kijana wa kike ni vigumu mawazo yako kukubaliwa; wazee wetu wa mtaa

[57] Ibid., p. 6
[58] Ibid.
[59] UN Women, “From Where I Stand: Young people do care, and we have expectations of what we want in our communities and from our government”, November 2022.
[60] In interviews with youth leaders, Kwale, August 2023.
[61] Interview with youth leader, Kwale, August 2023.

hawakusikilizi”[62]. Kulingana na ushuhuda wake, hata hivyo, nadharia hizo zinabadilika taratibu, kadiri vijana wengi zaidi wanavyojihusisha na siasa.

Itikadi hizi haziwaathiri vijana wa kike na wa kiume katika hali sawa; badala yake zina athari mbaya zaidi kwa wasichana. Kukosekana kwa usawa, hata hivyo, ni suala lenye sura mbili. Kwa mfano, wakati wengi wa waliohojiwa wanaamini kuwa wanawake wana fursa sawa za kushiriki katika jamii kama walivyo nayo wanaume, bila kuwepo tofauti kubwa kati ya wahojiwa wa kike na wa kiume, tafiti nyingi zinathibitisha kuwa wanawake wana uwakilishi mdogo katika karibu nyanja zote za maisha, ikiwemo elimu, uongozi wa kisiasa na kushiriki katika vyombo vya juu vya maamuzi. Hili siyo tu linaashiria kuwepo kwa mfumo dume, lakini pia kuwepo kwa sheria na desturi za kibaguzi na upendeleo uliokithiri wa kitamaduni[63]. Kwa sabau hiyo, ni muhimu kuonesha kuwa, mnamo mwaka 2022, Kaunti ya Kwale ilizindua Mpango Kazi wa Kaunti (CAP) uliochota kutoka Mpango wa Kitaifa (NAP) wa Kenya kuhusu Wanawake, amani na Usalama. Mpango huu unaweza kusaidia kuchochea mipango maalum ya ushirikishwaji wa wanawake katika masuala ya amani na usalama.

[62] Ibid.
[63] Centre for Human Rights and Policy Studies (CHRIPS), “Conflict Assessment Report: Danida Peace, Security and Stability (PSS) Programme, Kenya 2016-2020”, June 2017, p. 66.


# MOMBASA

## Aina za migogoro na miundo ya vurugu

Kukosekana kwa usalama ni tatizo kwa wakaazi wa Mombasa na hofu ya kutokea vurugu inaonekana wazi. Aina kuu ya migogoro inayotokea Mombasa ni uhalifu wa kutumia nguvu, hasa ule unaofanywa na makundi ya kihalifu ya vijana. Vichochezi vikuu vya vurugu ni kukosekana kwa usawa wa kiuchumi na kutengwa kwa jamii, ambavyo vinaonekana kuwasukuma vijana waliochanganyikiwa na wasio na kazi kujiunga na makundi ya kihalifu.

Kaunti ya Mombasa ipo katika eneo la kimkakati na ndio mji wenye bandari kubwa zaidi ya Kenya. Shughuli kuu za kiuchumi za kaunti hii ni pamoja na utalii, uvuvi, shughuli za usafirishaji wa baharini, na kuagiza na kuuza bidhaa nchi za nje kupitia bahari ya Hindi. Sehemu kubwa ya wakazi pia inategemea kilimo kwa ajili ya maisha yao[64]. Pamoja na kwamba kiwango cha elimu katika kaunti ya Mombasa kipo juu, kikiwa katika asilimia 86%[65] ya wakaazi wote, Mombasa inakabiliwa na changamoto ya ukosefu mkubwa wa usawa miongoni mwa raia wake na ukosefu wa ustawi wa pamoja[66]. Umaskini uliokithiri unaoambatana na utajiri mkubwa uliopo Mombasa unazusha chuki na hisia za kutengwa na kukosekana kwa usawa[67].

### Jadweli 3. Watu wanaosema matukio ya vurugu hutokea mara kwa mara katika maeneo wanayoishi




---

[64] Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), "Rapid Conflict Assessment-Mombasa County", 2021, p. 3.
[65] Centre for Human Rights and Policy Studies (CHRIPS), "Conflict Assessment Report: Danida Peace, Security and Stability (PSS) Programme, Kenya 2016-2020", June 2017, p. 73.
[66] UN Kenya, "Leave No One Behind: Peace and Conflict Analysis", March 2022, p. 13.
[67] Centre for Human Rights and Policy Studies (CHRIPS), "Conflict Assessment Report: Danida Peace, Security and Stability (PSS) Programme, Kenya 2016-2020", June 2017, p. 75

Wakati hali ikionekana kuimarika katika miaka ya hivi karibuni, usalama mjini Mombasa bado unaendelea kuwa changamoto na jambo linalowapa wasiwasi wakaazi wake. Asilimia 37% tu ya wanawake na 42% ya wanaume waliohojiwa katika utafiti wameonesha kujisikia salama kutembea katika maeneo yao ya jirani; ambapo asilimia 60% ya wanawake na 54% ya wanaume wanadhani kwamba matukio ya ukatili bado ni jambo la kawaida katika maeneo wanayoishi, hasa uhalifu, ikifuatiwa na unyanyasaji wa majumbani na ujambazi. Rudia jadweli nambari 3 hapo juu.

Kama ilivyo Kwale, tatizo kubwa lililoainishwa na wahojiwa wa Mombasa ni kuhusiana na makundi ya vijana wa mtaani. Makundi haya yanaendeleza shughuli zao bila kuadhibiwa na, ingawa sheria imepitishwa dhidi yao na kupigwa marufuku, ukuaji wao na kutapakaa kunafanya iwe vigumu kwa polisi kudhibiti hali hii[68]. Kwa hakika, baadhi ya ripoti zinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la vijana hivi karibuni kujiunga na makundi ya uhalifu na kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu katika pwani ya Kenya, ikiwa ni pamoja na Mombasa[69], na makundi haya yamekuwa yakitumika kama askari wa miguu katika biashara ya madawa ya kulevya mjini Mombasa[70]. Hili linayafanya makundi hayo pia kutumika kama chombo cha udhibiti wa kisiasa: ambapo katika kila duru ya uchaguzi vijana wanatumiwa na wanasiasa katika kuwania nafasi za kisiasa na wakati mwingine hata hulipwa ili kuwatishia wapinzani na kuonesha hasira zao katika mikutano ya hadhara.

Makundi ya kihalifu yapo sana katika maeneo ya Kisauni na Likoni, ambazo ni kaunti ndogo zilizofikiwa na mradi huu. Wengi wa wafuasi wa makundi haya ya vijana ni wale walioacha shule za msingi na vijana wasio na ajira na ambao wapo katika uraibu wa mihadarati[71]. Vijana wasio na ajira, wavivu na maskini wako katika hatari kubwa zaidi ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya na mihadarati. Wafuasi wadogo wenye umri wa mnamo miaka 7 hukusanya taarifa wakati wale wakubwa, wengi wao wakiwa baina ya miaka 10-20, wakiwa na visu na mapanga, hufanya mashambulizi. Mara nyingi hufanya uhalifu huo wakiwa wametumia dawa za kulevya, ili kupata "ujasiri na kujiamni" katika kutenda uhalifu[72]. Baadhi ya watoto hawa ni mayatima, na wengine wanajaribu kusaidia familia zao na hivyo kulazimika kufanya uhalifu wa kikatili, kama alivyoeleza aliyewahi kuwa mshiriki wa kundi la kihalifu: “Tunalazimika kutunza familia zetu na tunaweza kufanya hivyo tu kwa kuwapatia wazee wetu kiasi fulani cha fedha”[73]. Umaskini ndio sababu kubwa inayowasukuma vijana hawa kujihusisha na makundi ya kihalifu. Ugunduzi huu unaungwa mkono na takwimu za kiuchumi, kwani Mombasa imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa ajira ikilinganishwa na wastani wa kitaifa, kwa kiwango cha kati ya asilimia 44% mpaka 66% ikiwa pia itajumuisha watu wenye ajira isiyo rasmi, isiyo na usalama wala mazingira mazuri ya kazi.

---

68 Gumba D., “Gangs still drive Mombasa’s narco-city image”, Institute for Security Studies (ISS), September 2020.
69 Search for Common Ground, “Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa County”, December 2020, p. 5.
70 Gumba D., “Gangs still drive Mombasa’s narco-city image”, Institute for Security Studies (ISS), September 2020.
71 Search for Common Ground, “Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa County”, December 2020, p. 5.

72 Gumba D., “Gangs still drive Mombasa’s narco-city image”, Institute for Security Studies (ISS), September 2020.
73 Ahmed M., “Inside the Deadly Gangs of Mombasa”, Nation, August 2019.

Kama ilivyojitokeza Kwale, kutokana na changamoto zinazoletwa na makundi ya vijana wa mitaani, waliohojiwa wengi wanawaona vijana kuwa ni tishio la usalama. Na kwa maana hiyo, kuna mvutano mkubwa kati ya maafisa wa usalama na makundi ya vijana, kama ilivyo kati ya vijana na jamii zao[74]. Lakini, ikiwa vijana ni wahalifu kwa upande mmoja, wao pia ni kundi lililo hatarini zaidi kwa upande mwingine, kwa kuwa wanaelemewa kupita kiasi na ukosefu wa usalama wa kijamii na kiuchumi na mara nyingi wao wenyewe ni waathirika wa unyanyasaji[75].

Hali ngumu ya kiuchumi na ukosefu wa fursa za masomo sambamba na matumizi mabaya ya dawa za kulevya zinaonekana kama sababu kuu zinazochochea vurugu za makundi ya vijana[76]. Watoto na vijana wengi huacha shule na kujiunga na makundi haya wakitumaini kupata rasilimali za kiuchumi wanazohitaji. Mfuasi mmoja mdogo wa kundi la mtaani anaeleza: “Hii ndiyo njia pekee ya kupata pesa: tunalazimika kushambulia watu ili tuweze kujifaidisha kwa tunachokitaka”. Katika hali hii, uwajibikaji wa mamlaka za serikali na vyombo vya usalama, unaweza kuonekana kutokuwa na maana, na kuchangia, badala ya kudhibiti, katika kusababisha matatizo zaidi. Polisi hasa mara nyingi inaonekana kukosa uaminifu, kutokuwa na uwezo na kugubikwa na ufisai. Pia kuna madai kwamba polisi wanahusika katika ukiukaji wa haki za binadamu[77].

Aina nyengine kuu ya migogoro inayoathiri kaunti ya Mombasa, hasa Kisauni ni migogoro ya ardhi. Migogoro hiyo inachochewa na ushindani katika kupata rasilimali chache za ardhi na maji, ambazo huwagombanisha wafugaji na wakulima[78]. "Suala la ardhi ndio changamoto kubwa inayojitokeza mara kwa mara ambayo ofisi yangu hushughulikia", anaeleza mwakilishi wa serikali ya kaunti[79]. Migogoro hiyo inahusiana zaidi na ukosefu wa umiliki salama wa ardhi kwa watu wa asili wa pwani katika maeneo ambayo kuna mkusanyiko mkubwa wa watu wa kiasili wasio na ardhi[80]. Migogoro hii pia inahusishwa na kuchochewa na kukosekana kwa usawa tangu enzi za utawala wa Waarabu na Waingereza, ambao umeathiri mzunguko wa kihistoria wa ugawanaji wa ardhi, kwa kupendelea baadhi ya makundi kwa gharama ya wengine, na hivyo kufanya kuwepo kwa malalamiko ambayo yanaendelea hadi leo[81].

Kuhusu suala la vurugu za misimamo mikali, wakati Mombasa inatambuliwa katika nukuu nyingi kama kitovu cha misimamo mikali[82], wanajamii wanaonekana kuliangalia jambo hilo kama si muhimu sana.

---

[74] In interviews with youth and religious civil society organisation representatives, Mombasa, August 2023.
[75] Search for Common Ground, “Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa Count”y, December 2020, p. 6.
[76] In interviews with youth leaders, Mombasa, August 2023.
[77] Search for Common Ground, “Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa County”, December 2020, p. 7.
[78] Interiew with youth civil society representative, Mombasa, August 2023.
[79] Interiew with local government representative, Mombasa, August 2023.
[80] National Crime Research Centre, Crime and Violence Prevention Training (CVPT), “Mombasa County: Crime And Violence Rapid Assessment”, June 2017, p. 20.
[81] Ibid.
[82] Centre for Human Rights and Policy Studies (CHRIPS), “Workshop Note No.5: Countering and Preventing Violent Extremism in Mombasa County: Youth and Gender differentiation”, October 2020, p. 1.

Hii inapelekea kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya mitazamo ya jamii na vyombo vya usalama kuhusu suala hili. Pamoja na hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa Mombasa ina Mpango wa Utekelezaji wa Kaunti (CAP) wa kuzuia na kukabiliana na itikadi kali. Mpango huu ulianzishwa kupitia mchakato wa kushirikisha wadau mbalimbali na kuzinduliwa mwaka 2017, na unatarajiwa kumalizika mwaka huu. Hadi kufikia leo hii, mpango huu unatajwa kuwa mfano mzuri kwa raia na ushirikishwaji wa jamii.

## Viunganishi na vigawanishi

Walipoulizwa kuhusu viunganishi vikuu katika jamii, wanaume kadhaa waliohojiwa walitaja michezo. Kwa mujibu wa mwakilishi wa taasisi kubwa ya kiraia: "Kisauni imeunganishwa zaidi kupitia mpira wa miguu". Ameeleza mwakilishi huyo kwamba wavulana hasa hucheza mpira wa miguu kila siku na, kadiri inavyowezekana, wanapenda kwenda kuangalia michezo pamoja kwenye TV[83]. Wanawake kwa upande mwengine wanasisitiza kwamba mikusanyiko ya kijamii na sherehe ni matukio yanayoimarisha mahusiano ya watu, ikiwa ni pamoja na, kwa mfano, harusi, mazishi, mabaraza, na pia vikundi vya mikopo vya vijijini, mikusanyiko ya wanawake na vijana pekee, na sherehe za kidini.

Siasa na ukabila ndio vigawanishi vinavyotajwa mara nyingi, na aghalabu huhusishwa na upendeleo, ukosefu wa usawa na ubaguzi unaozingatia ukabila, uhusiano wa kisiasa na tabaka la kijamii. Ripoti na mahojiano yanaonesha kuwa siasa katika kaunti ya Mombasa zimejengeka katika misingi ya kikabila, na kwamba wanasiasa hutumia uhasama wa wazi uliopo na uliofichika wa kikabila kuzitishia jamii fulani, na kusababisha machafuko baadhi ya wakati. Wanasiasa wanatumia ukabila na hali mbaya ya kiuchumi ya watu kama karata ya uchaguzi badala ya kuwezesha maendeleo ya kisiasa na maslahi ya kaunti[84]. Masimulizi haya ya kibaguzi, yanayowatenganisha Wakenya wenye asili ya Kiarabu na wale ambao si Waarabu wala Waswahili, yanatokana na mifarakano ya muda mrefu iliyopo kati ya Waarabu na wasio Waarabu huko Mombasa[85]. Hisia hizo pia zinaweza kutanuka na kuhusisha jinsi gani rasilimali zote zinajadiliwa, zikiwemo ardhi na fedha za maendeleo.

| VIUNGANISHI | VIGAWANISHI |
|---|---|
| Michezo (hasa mpira wa miguu) | Siasa |
| Mikusanyiko ya kijamii (harusi, maziko, baraza, vikundi vya mikopo vya vijijini, vikundi vya wanawake na vijana, mikutano ya pamoja ya dini mbalimbali, sherehe za kidini, siku za kumbukumbu) | Ukabila |
| Utamaduni wa kiswahili | Upendeleo |

[83] Interiew with youth civil society representative, Mombasa, August 2023.
[84] Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), "Rapid Conflict Assessment: Mombasa County", 2021, p. 4
[85] International Organization for Migration (IOM), "Community-led Conflict Assessment Report: Mombasa, Kilifi, Lamu and Tana River Counties", November 2021, pp. 2-3.

| | |
|---|---|
| Dini | Hali ya kutokuwepo usawa na ubaguzi (kwa sababu ya ukabila, imani ya kisiasa, tabaka la jamii) |
| | Kukosekana fursa za kiuchumi |
| | Kukosekana usawa katika mgawanyo wa fedha za maendeleo |

## Uchambuzi wa wadau na uhusika wao

Zoezi la uchambuzi wa wadau lilifanyika kama sehemu ya uchambuzii wa migogoro ili kutambua wahusika wakuu katika migogoro na mienendo ya amani katika Kaunti ya Mombasa. Sehemu hii inatoa maelezo ya kila mmoja kati ya makundi makuu yaliyotambuliwa, ikiwa ni pamoja na maelezo ya ziada yaliyopatikana juu ya mitazamo na matendo.

### Mamlaka za serikali

Majukumu muhimu katika kaunti ya Mombasa yanatekelezwa na viongozi wa jamii na wazee, ambao wanachukuliwa na mamlaka za mitaa kama watu wanaoaminika na kuheshimiwa, ambao wanaweza kuratibu na kutoa huduma kwa wananchi, kuwasaidia kutekeleza majukumu yao[86]. Ukweli kwamba watu hawa - wazee au viongozi wa jamii - huchaguliwa na wanajamii wenyewe unapelekea kuhakikisha kiwango fulani cha ukaribu kati ya mamlaka za serikali na raia, jambo linalosaidia kuongeza mtangamano wa kijamii. Wazee, kwa mfano, wana jukumu la kuongoza mabaraza ambapo hujadili masuala muhimu ya kijamii, kiuchumi na kiusalama pamoja na washiriki wote. Katika mikutano hii, wazee na viongozi wa mitaa huishirikisha jamii kwa kutoa taarifa zinazohusiana na masuala ya usalama ambazo zimetoka serikalini, sambamba na kukusanya madhila yanayowakumba wanajamii. Mikusanyiko hii ya kijadi inatoa fursa kwa serikali kukutana kiurahisi na wadau husika katika ngazi ya jamii[87] na asasi za kiraia[88].

Vyombo vya usalama vinaheshimiwa, lakini bado haviaminiwi kikamilifu. Waliohojiwa wanathamini juhudi zinazochukuliwa na serikali za kuimarisha usalama mjini Mombasa, kwa mfano, kwa kuunda kamandi inayosimamia ulinzi na usalama wa maeneo muhimu ambayo uhalifu na shughuli za makundi maovu zimeripotiwa[89]. Waliohojiwa pia wametaja athari chanya za polisi-jamii, mbinu inayoimarisha ushirikiano kati ya polisi na jamii katika kupunguza uhalifu, machafuko na ukosefu wa usalama katika maeneo jirani. Polisi ya Kenya inaitafsiri mbinu hii kama "njia ya kiulinzi inayotambua uhuru na wajibu

---

[86] Kisia A., “Village elders could earn up to Sh12,000 monthly”, The Star, July 2023.
[87] Interview with youth civil society representative, Mombasa, August 2023.
[88] Interview with local government representative, Mombasa, August 2023.
[89] National Crime Research Centre, Crime and Violence Prevention Training (CVPT), “Mombasa County: Crime And Violence Rapid Assessment”, June 2017, p. 41

wa pamoja kati ya Polisi na Jamii katika kuhakikisha mazingira salama kwa raia wote"[90]. Polisi jamii ni mbinu ya kipolisi inayojielekeza katika mahitaji ya jamii, na kuchangia udhibiti wa migogoro ambapo doria za polisi huungwa mkono na kushirikisha majirani na raia. Mbinu hii kwa kiasi fulani inaweza kupunguza mtazamo hasi juu ya baadhi ya matendo ya polisi, ambayo, kwa mujibu wa wawakilishi kadhaa wa asasi za kiraia, hutumia nguvu nyingi bila ya kufanya uchunguzi wa kina[91], na hivyo kuwakatisha tamaa waathirika kuripoti matukio ya uhalifu kwa mamlaka[92]. Kwa ujumla, vyombo vya usalama bado vinakabiliwa na kiwango kikubwa cha kutoaminika. Ni asilimia 55% tu ya jinsia zote mbili waliohojiwa katika utafiti huu wanaoshawishika kuwa vyombo vya usalama vinawajibika, vinathamini na kuheshimu haki za binadamu.

## Asasi za kiraia

Katika kuangalia nafasi ya asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kukabiliana na machafuko mjini Mombasa, asilimia 91% ya wanawake na asilimia 82% ya wanaume wanaamini kuwa bila shaka asasi na mashirika ya kiraia yana jukumu muhimu katika kutatua migogoro kati ya jamii au makundi. Mtazamo huu unaakisi maneno ya wahojiwa wanaotambua mchango mkubwa wa AZAKi katika suala la amani na maendeleo[93], wakisisitiza kwamba asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya serikali yanakuza uhusiano mzuri wa jamii[94] na yanaonekana kuwa na msaada mkubwa[95]. Asasi za kiraia hufanya kazi ya kujenga uelewa wa jamii kuhusu masuala muhimu kama uongozi na afya na mara nyingi huratibu ushiriki wa jamii katika majadiliano ya kijamii, kiuchumi na kiusalama. Kwa maneno ya mwakilishi wa serikali, asasi za kiraia "zinafanya majadiliano ya amani, kupanda miti, mikoko, na kutumia fursa hiyo kuhubiri amani nchini"[96]. Muhimu zaidi, kutokana na nafasi ya makundi ya kihalifu Mombasa, kuna asasi zinazotoa huduma za kisaikolojia na kijamii na shughuli za kusaidia kuwarejesha wahalifu katika hali ya utu wa kawaida[97]. Hili linafanyika katika mazingira ambayo, vinginevyo, hakuna msaada wa namna hiyo kwa vijana walio katika hatari ya kujiunga, au kujaribu kuachana na makundi ya uhalifu[98] au ya wanamgambo. Asasi ambazo zimetajwa zaidi na waliohojiwa ni pamoja na *Humanity Action Knowledge Integrity in Africa* (HAKI Africa), *Swahilipot Hub*, Baraza la Maimamu na Wahubiri wa Kenya (CIPK) na *Stretchers Youth Organization* (SYO).

[90] Kenyan Police define community policing as “an approach to policing that recognizes the independence and shared responsibility of the Police and the Community in ensuring a safe and secure environment for all citizens” (source: Kenya Police Service).
[91] Interview with religious civil society organisation, Mombasa, August 2023
[92] Interview with youth civil society representative, Mombasa, August 2023.
[93] KII with youth civil society representative, Mombasa, August 2023
[94] KII with religious civil society organisation representative, Mombasa, August 2023.
[95] In KIIs with civil society representatives and government representatives, Mombasa, August 2023.
[96] KII with local government representative, Mombasa, August 2023.
[97] KII with youth civil society representative, Mombasa, August 2023.
[98] Search for Common Ground, “Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa County”, December 2020, p. 7.

## Vijana

Ushirikishwaji wa vijana na wanawake kwa hakika unaongezeka, lakini bado kuna vikwazo kwa ushiriki wa vijana, na waliohojiwa wanafahamu sana changamoto hizi[99]. Kwa mfano, kiutamaduni vijana wanachukuliwa kuwa hawana uwezo wa kufanya maamuzi na mara nyingi hupuuzwa kwa sababu watu wazima na wazee wanadhani na kushawishika kuwa wao pekee ndio wanajua kila kitu[100]. Mahusiano kati ya rika mara nyingi huwa na mvutano, jambo ambalo linaleta ugumu zaidi kwa vijana kuzungumza na kutoa mchango hasi kwa jamii yao. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa kunyamazia ufisadi na ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na vikosi vya polisi, serikali inachochea hasira na chuki kwa vijana. Vijana wengi wanadaiwa kuwekwa kizuizini kwa miezi kadhaa bila ya kufunguliwa mashtaka na kumekuwa na visa vya watuhumiwa kupigwa risasi na kuuawa ovyo katika Mwambao wa Pwani, mara nyingi kwa kisingizio cha kukabiliana na uhalifu[101]. Changamoto nyingine iliyotajwa na waliohojiwa ni kinyanganyiro kikubwa linapokuja suala la fursa zinazopatikana kwa vijana, ikisisitizwa kuwa "mara nyingi vijana wapo mara tano zaidi ya fursa yoyote inayotangazwa"[102].

Kama hali ilivyo kwa kaunti ya Kwale, kuna mkinzano wa kimtazamo ambao unapaswa kuripotiwa. Wahojiwa wakuu wanatambua kwamba vijana mara nyingi wanakosa kushirikishwa ipasavyo, lakini, kwa upande mwengine, kuna wanaopinga vikali mtazamo huo na kuamini kuwa ni uamuzi wa vijana wenyewe kutojishirikisha[103], na kwamba "wenyewe wanapenda kubaki kama walivyo kwani hawajaribu kufanya chochote cha maana kwa maslahi yao"[104] na kwamba "madawa ya kulevya yanawafanya vijana kutokuwa na maana katika jamii"[105]. Mtazamo huu unapaswa kufikiriwa na kutiliwa maanani. Kwa hakika mchango wa vijana katika amani na usalama unaelezwa kwa kiwango cha chini sana. Hata hivyo, ni muhimu sana kufahamu kwamba vijana tayari ni mabalozi wa mabadiliko waliojitolea na wenye uwezo mkubwa wa kuzuia vurugu na kushughulikia migogoro makhususi katika ngazi ya jamii.

Kuna vikundi vya vijana na taasisi zinazofanya kazi katika kujenga amani, kwa mfano Shakirina Youth for Development (SYD), ambayo inawawezesha vijana kama washirika sawa katika kuchangia maendeleo ya jamii zao. Taasisi hii ni ya kipekee kwa kuwa wanawake vijana ndio walio mstari wa mbele katika kutekeleza shughuli za msingi za taasisi, katika muktadha ambao kiujumla ni wa kihafidhina. Mfano mwingine mzuri ni taasisi ya Likoni Development Programme (LICODEP)[106] na mtandao wake wa vikundi vya vijana vinavyofanya kazi Mombasa na Kwale. Lengo la LICODEP ni


---

[99] In KIIs with civil society representatives, Mombasa, August 2023.
[100] Search for Common Ground, "Policy Brief: Promoting Youth Participation in Peace and Security Efforts in Mombasa County", December 2020, p. 7.
[101] Ibid.
[102] KII with local government representative, Mombasa, August 2023.
[103] Interview with civil society representative, Mombasa, August 2023.
[104] Interview with civil society representative, Mombasa, August 2023.
[105] Interview with government representative, Mombasa, August 2023.
[106] Olawale I., Youth, "Peace and Security in Kenya", December 2017, p. 22.

kuifanya jamii isikilize sauti za vijana na wanawake na kushughulikia mahitaji na changamoto zao katika mtazamo wa usawa wa kijinsia na kujenga amani. Miongoni mwa waliohojiwa, kiongozi kijana pia alitaja taasisi ya Youth Advisory Group (YAG)[107]. YAG iliundwa mwaka 2021, wakati taasisi ya Swahilipot Hub ilipokuwa mshirika katika Global Opportunity Youth Network (GOYN), mpango wa wadau mbalimbali unaolenga kuleta mabadiliko ya kimfumo yanayoendana na mahali kwa ajili ya fursa za kiuchumi kwa vijana. YAG inajumuisha vikundi vya vijana kutoka kaunti ndogo sita za Mombasa, na jukumu lake ni kuhakikisha kuwa sauti za vijana zinasikika. Wanachama wa YAG huandaa matukio, kushiriki katika kubuni njia za utatuzi wa changamoto za kijamii, na kutekeleza majukumu ya kimkakati ya utetezi kwa taasisi washirika, huku wakishiriki karibu kila siku katika mchakato wa kufanya maamuzi kwa niaba ya vijana wa Mombasa.

Cha kuvutia zaidi ni kwamba, miongoni mwa waliohojiwa, asilimia 66% ya wanawake na 58% ya wanaume wamethibitisha kuwa wanafahamu Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama; na asilimia 91% ya wanawake na 88% ya wanaume wanafahamu sera za serikali za kusaidia ushiriki na ustawi wa vijana, na kuonesha uelewa wa hali ya juu, hasa kwa wanawake, katika maeneo yote yaliyochambuliwa nchini Kenya na Tanzania. Wakati haikuwa wazi kufahamu sababu ya mwamko huo mkubwa, kwa hakika hili ni jambo linalopaswa kutumika katika utekelezaji wa mradi huko Mombasa. Jambo lililo na hakika ni kwamba kuna shauku kubwa ya vijana katika kutekeleza jukumu kubwa zaidi, katika amani na usalama, na katika maisha ya jamii kwa ujumla.

**Jadweli 4. Watu waliosema wamewahi kusikia kuhusu UNSCR 2250 juu ya Vijana, Amani na Usalama**




Inapoangaliwa nafasi ya makundi mengine yanayopaswa kujumuishwa katika mipango ya kuzuia migogoro na kujenga amani, wahojiwa mara nyingi wametaja watu wenye ulemavu (PWD) kwa

[107] Interview with youth leader, Mombasa, August 2023.

sababu hawapati nafasi sawa za ushiriki na wengi wao wametengwa katika michakato ya kufanya maamuzi[108]. Watu wenye ulemavu[109] nchini Kenya wanawakilisha karibu asilimia 10% ya watu wote, huku wengi wao wakiishi maeneo ya vijijini na wakiwa na umri wa chini ya miaka 24. Licha ya juhudi za kitaifa zilizochukuliwa kwa kuanzisha Baraza la Kitaifa la Watu Wenye Ulemavu mwaka 2004, kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) mwaka 2008, na kutambua haki za watu wenye ulemavu mwaka 2010, bado watu wenye ulemavu nchini Kenya wanakabiliwa na changamoto nyingi na uyanyapaa wa hali ya juu.

Kundi jingine linalonyanyapaliwa na kutengwa ni la watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja (LGBTQI+) ambao wanachukuliwa kuwa ni watu wa ajabu na kudharauliwa[110] na hivyo kukumbana na unyanyasaji na ubaguzi, kupata huduma za kijamii na afya kwa tabu, kushambuliwa na makundi ya watu, kusababishiwa vurugu, kukamatwa mara kwa mara na kufukuzwa nyumbani, shuleni na maeneo ya jirani[111]. Ikiangaliwa matukio ya hivi karibuni, Kenya imeshuhudia maandamano kadhaa dhidi ya LGBTQI+ baada ya Mahakama Kuu kuridhia kuwa jamii ya LGBTQ+ ina haki ya kujumuika[112]. Mnamo mwezi Machi 2023, kwa mfano, makumi ya watu wa jamii ya LGBTQI+ waliondoka Mombasa kufuatia tangazo la maandamano hayo, wakihofia usalama wao. Mashirika kadhaa yasiyo ya kiserikali yanafanya kazi ya kuwalinda watu wa jamii hii hasa kutokana na vurugu na unyanyasaji unaofanywa na jamii na polisi dhidi yao[113], lakini bado hakujakuwa na mpango makhsusi wa kuwashirikisha katika mazungumzo yanayohusu amani na usalama.

Suala jengine lililoibuliwa na mwakilishi wa serikali kutoka Kisauni ni kutengwa kwa jamii ya watu wenye asili ya Pemba nchini Kenya katika takriban huduma zote za kijamii[114]. Wapemba[115] ambao asili yao ni wavuvi kutoka kisiwa cha Pemba Zanzibar nchini Tanzania wanadai kuwa walifika Kenya kabla ya Vita vya Pili vya Dunia lakini mara nyingi wamekuwa hawana nyaraka [za utambulisho]. Kwa sababu hii, hawawezi kupata huduma muhimu za serikali. Kwa hakika hali ya jamii ya watu hawa iliimarika baada ya Rais wa Kenya Ruto kuwatangaza kama kabila jipya na kuwapa hati rasmi, lakini hali hiyo inapaswa kuendelea kufuatiliwa ili kuhakikisha ushiriki wao mkubwa.

## NAFASI YA UTAMADUNI WA WASWAHILI NCHINI KENYA

Kwa mujibu wa asilimia 7% ya wanawake na asilimia 95% ya wanaume waliohojiwa kutoka Kwale, Utamaduni wa Waswahili unawakilisha mfumo wa maisha katika jamii yao. Kwa upande wa

[108] An interviews with civil society representatives and youth leaders, Mombasa, August 2023.
[109] Global Disability Rights, "Disability in Kenya", 2023.
[110] UN Kenya, "Leave No One Behind: Peace And Conflict Analysis," March 2022, p. 17.
[111] The Gay and Lesbian Coalition of Kenya (GALCK).
[112] Kaledzi I., "LGBTQ+ Community in Kenya Defies Anti-Gay Protests", Deutsche Welle (DW), October 2023.
[113] UN Kenya, "Leave No One Behind: Peace And Conflict Analysis", March 2022, p. 17.
[114] In interview with local government representatives, Mombasa, August 2023.
[115] Okwembah N., "Pemba Tribe Destroys Fake Ids After Receiving Official Papers", The Standard, August 2023.

Mombasa asilimia ni 78% kwa wanawake na 85% kwa wanaume. Kwa mujibu wa waliohojiwa, utamaduni wa Waswahili unahusisha vyakula, mila na desturi, matukio ya kijamii kama vile ndoa, kanuni za mavazi na mwingiliano wa kijamii. Ukarimu ndio msingi mkuu wa utamaduni wa Waswahili, unaoakisi uchangamfu wa kiwango cha hali ya juu cha upendo wa jamii ya watu wa pwani. Utamaduni wa Waswahili pia unahusu, kwa upande mmoja, mtindo wa maisha yao ya upole, lakini kwa upande mwingine una uhusiano mkubwa na dini ya Kiislamu, pamoja na tabia zake na desturi za kijamii.

Utamaduni wa Waswahili unajidhihirisha zaidi katika mikusanyiko yake ya kijamii, kuanzia mabaraza hadi ndoa, sherehe za kidini hadi za kitamaduni ambapo watu hukutana, wakazungumza na kujadiliana masuala mbalimbali yanayowahusu. Neno Baraza lenyewe ni neno la Kiswahili linalomaanisha mkutano wa wazi kwa ajili ya kujenga uelewa, kujibu masuali ya jamii, kupeana taarifa muhimu na kushirikisha wananchi katika kutatua matatizo. Baraza pia zinatumika kama njia ya kusambaza habari kwa jamii na fursa ya kupokea maoni na maarifa juu ya masuala muhimu yanayoathiri jamii hiyo[116]. Baraza ni chombo muhimu sana katika kuimarisha mazungumzo kuhusu mabadiliko ya jamii[117].

Katika utamaduni wa Waswahili, maskani nazo ni sehemu muhimu za mikusanyiko. Katika maskani watu hukusanyika kwa njia isiyo rasmi ili kupumzika na kuamiliana[118]. Maskani ni sehemu ambazo huhudhuriwa zaidi na wanaume ambao hukaa pamoja, na kuzungumza kwa kubadilishana mawazo huku wakinywa kahawa au chai, kutafuna miraa, na kucheza michezo mbalimbali. Maskani ni karibu chanzo kikuu cha habari katika Pwani nzima ya Kiswahili.

Wahojiwa wengi wanaamini kuwa utamaduni wa Waswahili huchangia mtangamano wa kijamii miongoni mwa watu wake. Hiyo ni asilimia 87% ya wanawake na 90% ya wanaume kutoka Kwale na 72% ya wanawake na 78% ya wanaume kutoka Mombasa. Kwa maneno yao, utamaduni wa Waswahili una mchango mkubwa katika kukuza amani na mafungamano ya kijamii. Hili linadhihirika hasa wakati wa harusi na mikusanyiko ya kijamii ambapo watu hukusanyika kwa ajili ya kushereheka katika hali ya maelewano na umoja, wakisisitiza umoja na kujenga uhusiano usio na migogoro. Kwa mujibu wa mwakilishi kijana wa shirika la kiraia kutoka Mombasa, "utamaduni wa Waswahili umesaidia kuboresha mahusiano mazuri ya kujaliana, miongoni mwa wenyeji na wageni wakiwemo watalii"[119]. Mwakilishi wa taasisi ya kiraia ya Mombasa anaeleza kwamba AZAKi na jumuiya za ngazi ya chini zinatumia utamaduni wa Waswahili ili kujenga uelewa na kusambaza ujumbe wa amani[120]. Njia za kijamii za kutatua mizozo ya ndani ya jamii husika, lugha ya pamoja, na

---

[116] UN Uganda, “Human Rights Baraza: A Handbook on Conducting Community Public Meetings”, April 2014.
[117] In an interview with civil society representative, Mombasa, August 2023.
[118] Search for Common Ground, “Meet me at the Maskani: Mapping of Influencers, Networks, and Communication Channels in Kenya and Tanzania”, June 2017, p. 8.
[119] In interviews with youth leader, Mombasa, August 2023.
[120] In interviews with civil society representative, Mombasa, August 2023.

kushikamana na desturi za kitamaduni za jamii husika huimarisha zaidi uhusiano wa kijamii. Utamaduni wa Waswahili pia hurithisha maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine, hivyo basi unachukuliwa kama ni mfumo wa elimu unaoweka bayana maadili ya jamii yanayopaswa kuenziwa.

Kiujumla, utamaduni wa Waswahili unatumika kama msingi wa kujenga jamii yenye amani na iliyoungana. Kwa mujibu wa kiongozi wa kidini wa Kwale, "Kiswahili ni chombo muhimu cha utamaduni ulioshikana"[121] ambapo mwakilishi kutoka serikali ya mtaa anasisitiza kuwa, kwa maoni yake, dini na utamaduni zimefungamana sana na zote kwa pamoja zinahimiza amani[122]. Mjini Mombasa karibu watu wote waliohojiwa (asilimia 93% ya wanawake na 97% ya wanaume) wanaamini kwamba ni dini zaidi kuliko hata utamaduni wa Waswahili, inayoelezea kwa mapana mfumo wa maisha wa jamii za Mombasa.

Waliohojiwa wametaja vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Waswahili, kwa mfano nyimbo na mashairi ya kukemea vurugu na kuhamasisha amani na mshikamano, ambayo "kwa kawaida hujenga hisia na kukuza kujitafakari"[123], au umuhimu wa wazee ambao wanapaswa kuheshimiwa na kutiiwa. Heshima kwa wazee, hata hivyo, inaweza kuwa na utata katika suala la mahusiano baina ya rika tofauti, kwani vijana wamelalamika kwamba hawasikilizwi na wazee.

Zaidi ya hivyo , pamoja na kwamba utamaduni wa Waswahili kwa kiasi kikubwa unachukuliwa kuwa ni utamaduni wa amani, linapokuja suala la kuunga mkono usawa wa kijinsia, majibu ya wanaume na wanawake wa Kwale yanatofautiana kidogo. Asilimia 72% ya wanaume wanaamini kuwa utamaduni wa Waswahili unaunga mkono usawa wa kijinsia, ambapo ni 55% tu ya wanawake wanaoamini hivyo. Mjini Mombasa, asilimia 59% ya wanawake na 58% ya wanaume wanaamini hivyo.

Utamaduni wa Waswahili unazidi kupungua umuhimu kwa upande wa Kwale kwa mujibu wa asilimia 84% ya wanawake na 74% ya wanaume, lakini bado ni lazima uendelezwe na kuenziwa kwa mujibu wa maoni ya asilimia 84% ya wanawake na 88% ya wanaume. Kwa upande wa Mombasa ni asilimia 76% ya wanawake na 48% tu ya wanaume wanaoamini kuwepo kwa hali hiyo, huku asilimia 84% ya wanawake na 94% ya wanaume wakiamini kwamba kuna haja ya kuendeleza na kudumisha utamaduni huu. Baadhi ya waliohojiwa wameeleza kuwa mila za kiswahili zinaendelea kupotea[124]. Mwakilishi wa jumuiya ya vijana kutoka Mombasa anakiri, kwa mfano, kwamba siku hizi imekuwa ni nadra sana kwa wanafamilia kula chakula cha pamoja, jambo ambalo lilipewa umuhimu mkubwa sana hapo zamani.

---

[121] Interview with religious leader in Mombasa, August 2023.
[122] Interview with local government representative in Mombasa, August 2023
[123] Interview with youth civil society representative in Kwale, August 2023
[124] Interview with you leader in Mombasa, August 2023.

# TANZANIA

Tanzania inayochukuliwa kuwa nchi tulivu ikilinganishwa na jirani zake, imeendelea kushuhudia ongezeko la migogoro ya vurugu katika kipindi cha miongo miwili iliyopita. Nchi hiyo imefanya chaguzi za vyama vingi mara kadhaa tangu kuhama kutoka siasa za chama kimoja mwanzoni mwa miaka ya 1990, lakini chaguzi zimekuwa ni chanzo cha wasiwasi na machafuko nchini humo. Zaidi ya hayo, kuna mivutano ya kisiasa, kidini, na kiuchumi ambayo pia imechangia katika migogoro ya vurugu. Malalamiko ya kijamii na kisiasa na kutegwa kwa baadhi ya makundi kunachochea vurugu huku kupungua kwa nafasi ya raia kushiriki katika siasa kukitia dosari uhusiano kati ya serikali na wadau wengine, kupelekea baadhi ya watu binafsi na makundi kutumia njia za vurugu kujaribu kufikia malengo yao ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, au kidini[125]. Hata hivyo, maboresho yameonekana hivi karibuni chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameshika urais mwaka 2021[126]. Mwaka 2022, kwa mfano, serikali iliongeza uhuru wa vyombo vya habari na kurejesha leseni za magazeti kadhaa makubwa, ambayo yalipigwa marufuku au kusimamishwa hapo awali. Katika mwaka huo huo, Freeman Mbowe, mwenyekiti wa upinzani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alitolewa kutoka kizuizini baada ya mashtaka ya ugaidi dhidi yake kuondolewa. Na hivi karibuni, Serikali imetupilia mbali marufuku iliyokuwa imewekwa hapo awali kuhusu mikutano ya kisiasa.

Kuongezeka kwa wapiganaji wa misimamo mikali (VE) kumeathiri jinsi nchi inavyoshughulikia majadiliano ya amani na usalama[127]. Kuongezeka huku kwa kiasi kikubwa kunahusishwa na ukaribu uliopo wa Tanzania na Kenya na Somalia, ambapo makundi ya al-Qaeda na al-Shabaab wamepanua uwepo wao[128]. Na hivi karibuni pia kumekuwepo mpaka ulio wazi kati ya Tanzania na Msumbiji ambao unafanya iwe rahisi kwa watu wenye msimamo mikali kujipenyeza nchini. Hata hivyo, matukio ya wapiganaji wa misimamo mikali yameendelea kuwa chini ya uangalizi makini, ingawa uchochezi wa itikadi kali, kuingiza watu katika makundi ya itikai kali, na mashambulizi madogo madogo yamekuwa yakitokea nchini Tanzania, ingawa kwa kiasi kikubwa yanafichwa kwa jamii. Serikali ya Tanzania na vyombo vya usalama wanakataa kutambua kwamba idadi inayoongezeka ya mashambulizi ya ndani ni mfano wa itikadi kali, na wamekuwa wakiyatambulisha kama ni matendo ya kihalifu tu. Msimamo wa Serikali ya Tanzania unapewa nguvu na kujizuia, kwa kiasi fulani, kwa vyombo vya habari vya ndani na asasi za kiraia katika kujadili mada hiyo hadharani kwa hofu ya kudhibitiwa na serikali. Hivyo, kuna ufahamu mdogo wa umma kuhusiana na hali hiyo nchini Tanzania[129].

---

[125] Search for Common Ground, "Baseline and Conflict Assessment: Jenga amani Yetu", 2020.
[126] Freedom House, "Country Profile: Tanzania", 2023.
[127] Agency for Peacebuilding, "Final External Evaluation of the Jenga amani Yetu – Building peaceful communities in Tanzania project by Search for Common Ground", July 2022.
[128] United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 1.
[129] Ibid, p. 7.

Suala jengine la kitaifa la kuzingatiwa ni unyanyasaji wa kijinsia (GBV), ambao umeenea na ni maarufu nchini Tanzania. Unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa majumbani, na ukeketaji wanawake (FGM) ni mambo yanayofanyika sana, lakini mara chache kuchukuliwa hatua za kisheria. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 40% ya wanawake na wasichana nchini Tanzania wamepitia unyanyasaji wa kimwili, asilimia 17% wamekumbana na unyanyasaji wa kingono katika maisha yao, na asilimia 28% ya wasichana wamepitia unyanyasaji wa kingono kabla ya kuwa watu wazima[130]. Sheria na mila kuhusu ndoa, talaka, urithi na masuala mengine zinapendelea zaidi wanaume kuliko wanawake, hususan Zanzibar[131]. Licha ya changamoto hizi, au labda katika kukabiliana na changamoto hizi, Tanzania sasa inaendelea kuandaa Mpango Kazi wa Kwanza wa Kitaifa (NAP[132]) kuhusu Wanawake, Amani na Usalama (WPS). Tofauti na Kenya, hakuna sera kuu nyengine zinazoonesha dhamira ya nchi katika kushughulikia migogoro ya ndani na kujenga amani.




*Wanafunzi wadogo nchini Tanzania wakishiriki kampeni ya #VijanaNaamani255 (Picha kwa hisani ya Global Peace Foundation, 2023).*

[130] Embassy of Ireland in Tanzania, "Addressing GBV and Gender Inequality Through the Tanzanian Criminal Justice System", October 2020.
[131] Freedom House, "Country Profile: Tanzania", 2023.
[132] UN Women, "Involving Women in Peace and Security: Good Practices in the Implementation of 1325 National Action Plans in East and Southern Africa", November 2022.

# MTWARA

## Aina za migogoro na miundo ya vurugu

Licha ya kwamba, kwa mtazamo wa ujumla, Mtwara inaonekana kuwa mahali salama, ukatili wa majumbani na ukatili wa kijinsia ni matukio ya kushitusha kwa mujibu wa washiriki wa utafiti na vyanzo vingine. Aidha, migogoro ya ardhi na migogoro inayohusiana na madereva wa bodaboda inastahili kutajwa pia, kama ilivyobainishwa na washiriki.

Mtwara kwa muda mrefu imekuwa ni eneo lililotengwa ndani ya Tanzania, lililosahauliwa na serikali za kikoloni na baada ya uhuru, na kukabiliana na kutelekezwa kihistoria na kubaguliwa. Kilimo na ufugaji bado ndio njia kuu ya maisha kwa asilimia 90% ya wakaazi wake. Ugunduzi wa hivi karibuni wa gesi asilia, ambao ungepaswa kuleta mabadiliko mazuri kimaendeleo, umesababisha hali ya kutoridhika kwa wananchi. Matarajio ya jamii kuhusu utajiri na maendeleo hayakufikiwa, hivyo kuzidisha mvutano kati ya jamii na serikali.

Ukiachia hayo, ukanda huu wa Mtwara kwa sasa una kiwango fulani cha utulivu. Jitihada za nje na miradi ya maendeleo imetoa msaada mkubwa katika kupunguza mvutano wa kiuchumi, kijamii, na kisiasa[133]. Kati ya washiriki wa utafiti, asilimia 86% ya wanawake na 90% ya wanaume wameonesha kujisikia wapo salama kutembea katika maeneo ya jirani, huku asilimia 93% ya wanawake na 100% ya wanaume wakieleza kwa uhakika kuwa matukio ya vurugu hayapo kabisa katika maeneo wanayoishi. Zaidi ya hayo, kama ilivyoelezwa na mwenyekiti wa kijiji, kuna tofauti kubwa kati ya usalama na amani: kuwepo kwa kiasi kikubwa kwa vyombo vya usalama na doria za usalama ni ishara kwamba suala la usalama linapewa umuhimu mkubwa, lakini, wakati huo huo, uwepo wao unaonesha wazi kuwa hali kiujumla si ya amani[134].

Matukio maarufu zaidi ya vurugu huko Mtwara kwa mujibu wa washiriki wa utafiti ni unyanyasaji wa majumbani (asilimia 75% ya wanawake na asilimia 70% ya wanaume) na unyanyasaji wa kijinsia (asilimia 65% ya wanawake na asilimia 68% ya wanaume). Cha kuvutia ni kuwa, mahojiano na watoa taarifa 17 huko Mtwara, ambao nane kati yao ni wanawake, hawakutaja sana kuhusu unyanyasaji wa majumbani na wa kijinsia. Hii pia imejitokeza katika mazingira mengine yaliyotafitiwa. Hii inaweza kuhusishwa na ukweli kwamba bado kuna utata katika kuzungumzia masuala haya, kama vile ambavyo bado kuna hofu katika kuripoti unyanyasaji kwa vyombo vya usalama, kwani unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia bado unachukuliwa kama aibu na

[133] Agency for Peacebuilding, “Final External Evaluation of the Jenga amani Yetu – Building peaceful communities in Tanzania project by Search for Common Ground”, July 2022, pp. 8-9.
[134] This could be an indication of a situation of negative peace, where the presence of security forces has led to the reduction of conflict related to immediate causes. However, as structural causes of conflict remained unaddressed, positive peace still remains a faraway goal for the region.

waathiriwa wanakataa kutafuta msaada[135]. Hata hivyo, ukimya kwa watu waliohojiwa kuhusu kueleza unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuwa umetokana na jinsi maswali ya utafiti huu yalivyoundwa, yakielekeza zaidi washiriki kuzingatia "mazingira ya nje" ya vurugu na migogoro katika ngazi ya jamii na maeneo jirani, badala ya kuangalia ndani ya kaya, ambako unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi hutokea. Jambo la hakika linaloweza kusemwa ni kuwa migogoro ya ndani na ya wanandoa ipo kwa kiwango kikubwa sana Mtwara, kama baadhi ya waliohojiwa walivyokiri kuwa hii ni hali ya kawaida sana ambapo upatanishi na uweledi katika kuhibiti migogoro unahitajika, pamoja na migogoro ya ardhi, ambalo ni suala jengine nyeti katika nchi nzima[136].

Migogoro ya ardhi[137] ni jambo maarufu sana na kwa kiasi kikubwa linasababishwa na ushindani juu ya rasilimali chache za ardhi na maji, mapungufu na mikinzano katika sera na sheria zinazosimamia migogoro ya ardhi, uwakilishi wa kisiasa usio wa usawa katika taasisi, uongozi mbovu na ufisadi, ukiukaji wa haki za binadamu na ulishaji wa mifugo katika vilimo vya wakulima. Migogoro ya ardhi, inapochochewa na usimamizi mbaya wa ardhi kama huo, inachangia kutokea kwa vurugu na ni chanzo cha upotevu wa maisha, mali na kuvurugika kwa maisha ya watu[138]. Waliohojiwa wameonesha kutokuwa na ufahamu kuhusu sheria za ardhi, na watu kununua na kuuza ardhi bila kufuata taratibu za kisheria au kutozingatia mipaka kati ya viwanja au mashamba. Hii husababisha mvutano na mizozo kati ya wanajamii au baina ya vijiji. Pia kuna mgogoro mwingine kati ya wanajamii na serikali, hifadhi za mbuga au wawekezaji, ambao ni matokeo ya mawasiliano mabovu kati ya jamii na wadau hawa, au pale ardhi ya jamii inapochukuliwa bila ya kulipwa fidia sahihi[139]. Cha kuvutia ni kuwa kuna uhusiano kati ya ukatiki wa kijinsia na migogoro ya ardhi kwa kiasi fulani; kwa sababu mivutano ya vurugu hujitokeza zaidi wakati wa kugawana mirathi, hasa pale wanapohusika wanawake katika masuala haya.

Migogoro iliyoripotiwa ilihusisha pia tukio maalum la kufungwa kwa mpaka wa Namoto[140]. Kivuko hiki kinachounganisha Palma, upande wa Msumbiji, na Mtwara kwa Tanzania kilifungwa mnamo mwezi Aprili 2021 baada ya shambulio lililofanywa na waasi waliohusiana na Dola la Kiislamu. Mwakilishi wa Asasi za Kiraia[141] anaeleza kwamba kufungwa kwa mpaka kulileta changamoto siyo tu kwa harakati za watu, lakini zaidi kwa biashara. Kufungwa huko kulivuruga biashara ya mipaka kati ya nchi hizo mbili, ambayo inawakilisha sehemu muhimu ya uchumi[142] wa pande zote za mpaka. Hatimaye, mnamo Septemba 2023, lango hili muhimu la biashara lilifunguliwa tena[143]. Hata hivyo,

[135] Interview with a woman farmer in Mtwara, August 2023.
[136] In interviews with local government representatives and community leaders in Mtwara, August 2023.
[137] Mohamed A., "A Review on Unresolved Major Causes of Land Conflicts in Tanzania: A case of Kiteto District, Manyara Region", *International Journal of Research Publications* (IJRP), Vol.58, issue 1, August 2020, p. 17.
[138] Search for Common Ground, "Baseline and Conflict Assessment: Jenga amani Yetu", 2020.
[139] Ibid.
[140] Gould T., "Namoto border crossing reopens", Zitamar News, September 2023.
[141] Interview with civil society representative in Mtwara, August 2023.
[142] Makoye K., "Mozambique's insecurity endangers cross-border trade", Anadolu Agency, June 2022.
[143] Gould T., "Namoto border crossing reopens", Zitamar News, September 2023.

kutokuwepo kwa usalama kunakohusishwa na misimamo ya itikadi kali, pamoja na hatari ya uwezekano wa kufungwa tena siku za mbele, kunaleta changamoto kubwa kwa biashara ya mipaka, ikiathiri mwenendo wa bidhaa za viwandani na za kilimo, ikiwa ni pamoja na mahindi, korosho, pamoja na biashara ya mifugo, mbao na shughuli za uvuvi[144].

Mgogoro mwengine muhimu unawahusisha madereva wa bodaboda. Bodaboda ni baiskeli na pikipiki ambazo ni maarufu sana katika nchi za Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na Kenya na Tanzania. Waendeshaji wa bodaboda ambao hutoa huduma ya usafiri wa haraka na unaofikia maeneo ya ndani zaidi, siyo tu kwamba wanajaza pengo muhimu katika mfumo wa usafiri wa umma, lakini pia wanachangia katika uchumi wa eneo hilo, kwa kutoa fursa za ajira. Hata hivyo, kuna changamoto kadhaa zinazohusisha masuala ya usalama, usalama wa barabarani, ushiriki wa matendo ya kihalifu, na mivutano na wawakilishi wa vyombo vya sheria. Mivutano kati ya waendesha bodaboda na polisi, hasa, inaelezewa na wahojiwa kama suala la kuogopesha huko Tandahimba[145]. Madereva wa bodaboda, ambao aghalabu ni vijana, wameelezewa kama wachangiaji wa migogoro ya vurugu kutokana na kushiriki kwao katika migogoro mingi ya kisiasa na kijamii dhidi ya serikali, kama vile mivutano kati yao na polisi kuhusu sheria za barabarani na usalama[146].

Udereva wa bodaboda mara nyingi ni fursa pekee kwa vijana kupata kipato, hata hivyo madereva hawa mara nyingi hujikuta wakiwa aidha waathirika au wahalifu katika pirika zao za barabarani zinazohusisha uhalifu kama wizi, kusafirisha wezi au bidhaa zilizoibiwa, na usafirishaji wa vitu haramu[147]. Pia kuna wasiwasi unaoongezeka kutokana na ongezeko la uhalifu unaofanywa kwa kutumia pikipiki, ambapo mmoja wa waliohojiwa alisema kwamba vijana waendesha bodaboda pia wapo katika mgogoro na wakulima kwa sababu [wakulima] wanawashutumu waendesha pikipiki kwa kusafirisha bidhaa zilizoibiwa[148]. Hali hii inahitaji kudhibitiwa kwa umakini kwa sababu mara nyingi vijana hawa hawana hata leseni ya udereva au, kwa vyovyote vile, hawajajifunza vya kutosha sheria za usalama barabarani[149].

Kwa mara nyengine vijana wanatajwa kama kitovu cha vurugu na baadhi ya waliohojiwa hawafichi maoni hasi waliyonayo hidi ya vijana, kwamba wanawachukulia kama wavivu, wenye tamaa na wasiokuwa tayari kujipatia kipato chao kwa kufanya kazi na kwa uaminifu[150]. Maoni haya yaliyojiegemeza upande mmoja yanapelekea ugumu zaidi kuwashirikisha vijana walio hatarini zaidi na, kwa maana hiyo, kuna umuhimu kuonesha kwamba vijana ndio wanaoathirika zaidi na matatizo ya kiuchumi na ukosefu wa fursa kusini mwa Tanzania. Kwa namna fulani vijana wanajihisi kama vile hawana kitu cha kupoteza, kwa mujibu wa taarifa za watu kadhaa.

---

[144] Makoye K., “Mozambique’s insecurity endangers cross-border trade”, Anadolu Agency, June 2022.
[145] In interviews with farmers and entrepreneurs in Tandahimba, August 2023.
[146] Search for Common Ground, “Baseline and Conflict Assessment: Jenga amani Yetu”, 2020.
[147] The Citizen, “DC: ‘Boda Boda’ May Be Useful in Combating Crime”, March 2016.
[148] Interview with with woman farmer in Mtwara, August 2023.
[149] Interview with woman farmer in Mtwara, August 2023.
[150] In interviews with various informants in Mtwara, August 2023.

Mtwara inachukuliwa kuwa kitovu cha vurugu za itikadi kali, kutokana na mashambulizi makali yaliyotokea karibu na mpaka wa Tanzania na Msumbiji na harakati za makundi ya itikadi kali (VE) katika maeneo hayo[151], lakini hakuna hata mmoja kati ya washiriki wa utafiti aliyeleza moja kwa moja kuhusu itikadi kali au ugaidi kama aina ya mgogoro unaoathiri jamii yao. Katika miaka ya hivi karibuni, tawi la Dola la Kiislamu nchini Syria (ISIS) lililopo Msumbiji, lijulikanalo kama Al-Shabaab, linadhaniwa kuwa tishio kubwa kwa watu wanaoishi kando ya mpaka. Hata maafisa wa serikali ya Tanzania wamekiri hadharani shughuli za kigaidi katika eneo hilo, tofauti na msimamo wao wa awali wa kupuuza tishio hilo na kuliita kama "vurugu za wahuni". Utofauti katika taarifa unaashiria kuwepo kwa tofauti kubwa katika mtazamo wa jamii na serikali kuhusu changamoto zinazosababishwa na itikadi kali ikilinganishwa na aina nyengine za migogoro mikali[152].

## Viunganishi na vigawanishi

Ukiangalia kile kinachowaunganisha watu wa Mtwara, utakuta kuwa biashara imetajwa kuwa sababu kuwa ya kuunganisha watu, kwa mujibu wa baadhi ya wahojiwa[153]. Kwa maneno ya kijana anayefanya kazi Redio ya Newala: "Biashara ndiyo kiungo muhimu katika Wilaya ya Newala. Tunategemea kufanya biashara na watu kutoka kaskazini mwa Msumbiji na mikoa ya kusini mwa Tanzania[154]". Uuchumi himilivu ndio jambo kubwa linaloangaliwa na wanajamii, linalowaleta pamoja licha ya tofauti za mitazamo yao ya kisiasa na imani za kidini.

Sababu nyingine inayowaunganisha watu ni dini ya Kiislamu na Kikristo, kwa sababu wakati wa shughuli za kidini na kijamii kama mazishi, harusi, na siku nyingine za sherehe watu hukusanyika kwa amani. Pia, matukio ya kijamii kama vile tamaduni za jadi, muziki na matukio ya ngoma na michezo hutajwa na wanaohojiwa[155] kama viunganishi muhimu.

Siasa kwa upande mwengine inaelezewa kuwa miongoni mwa vitenganishi vikuu vya jamii huko Mtwara[156]. Hii inajitokeza zaidi wakati wa uchaguzi, ambapo wafuasi wa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), mara nyingi hukabiliana na wafuasi wa vyama vya upinzani, Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).
Ugumu wa maisha, bei duni za mazao ya biashara na umaskini uliokithiri pia huzidisha migogoro kati ya watu, na kati ya jamii na serikali kama ilivyojitokeza katika maandamano ya bomba la gesi la Mtwara, ambayo inaonesha wazi kuwa ikiwa raia watajihisi kutengwa na kutelekezwa katika

[151] U.S. Department of State, "Country Reports on Terrorism 2021, Tanzania", 2021.
[152] United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 8.
[153] In interviews with civil society, media and local government representatives in Mtara, August 2023.
[154] Interview with young journalist in Mtwara, August 2023.
[155] Interview with civil society and local government representatives in Mtwara, August 2023.
[156] Interview with civil society and local government representatives in Mtwara, August 2023.

mipango ya maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi, vurugu zinaweza kutokea[157]. Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa, ukosefu wa ajira hufanya watu, hasa vijana, kuwa dhaifu zaidi na hivyo kuwa tayari kushiriki katika vurugu ili kuweza kujikimu wao na familia zao[158].

| CONNECTORS VIUNGANISHI | VIGAWANISHI |
|---|---|
| Biashara | Siasa |
| Dini na sherehe za kidini | Umaskini na ukosefu wa ajira |
| Utamaduni wa jadi, ngoma, na michezo | |

## Uchambuzi wa wadau na uhusika wao

Zoezi la uchambuzi wa wadau lilifanyika kama sehemu ya uchambuzi wa migogoro ili kutambua wahusika wakuu wenye jukumu katika mienendo ya migogoro na amani katika Mkoa wa Mtwara. Sehemu hii inatoa maelezo ya kila kundi kuu lililotambuliwa ikiwa ni pamoja na maelezo ya ziada endapo yanapatikana juu ya mitazamo na matendo.

### Mamlaka za Serikali

Jumla ya asilimia 98% ya wanawake na 95% ya wanaume miongoni mwa washiriki wa utafiti wanaamini kuwa ni jukumu la mamlaka za serikali kutatua migogoro kati ya makundi ya jamii. Watu wa Mtwara wanaiangalia serikali, ikiwa ni pamoja na vyombo vya usalama, kwanza kabisa kwa kuhakikisha usalama wa mipakani[159]. Kwa ujumla, kwa mujibu wa vijana waliohojiwa, Serikali za mitaa ndizo zenye wajibu wa kwanza katika kutatua changamoto zinazowakabili wanawake (kwa mujibu wa asilimia 75% ya wanawake na 81% ya wanaume ya waliohojiwa) kuliko zile changamoto zinazowakabili wanawake na vijana (ambayo ni asilimia 61% ya wanawake na 63% ya wanaume). Wengi wa waliohojiwa wameeleza kuridhika kwao na ukweli kwamba mamlaka zinahakikisha kiwango cha kuridhisha cha usalama kwa raia. Kwa ujumla, wahojiwa wanaiamini zaidi serikali linapokuja suala la kuzuia vurugu, udhibiti wa mpaka, na ulinzi dhidi ya uhalifu na misimamo mikali. Hata hivyo, upande mwengine wa sarafu watu wanalalamikia udhibiti uliowekwa juu yao, ambao ni sehemu ya mipango ya usalama iliyowekwa katika eneo hilo. Vyombo vya usalama vinawajibika, vinaitika, na kuheshimu haki za binadamu, na hasa haki za vijana, kwa mujibu wa asilimia 61% ya wanawake waliohojiwa na asilimia 71 ya wanaume, ikionesha mtazamo uliopo wa jinsia ambapo wanawake vijana wanaonesha kuwa na imani ndogo kabisa na vyombo vya usalama kuliko ilivyo

[157] Mwesiga T. and Mikova K., "Mtwara Gas Project Conflict: Causes of Arising and Ways of Stabilization (Part 2)", Social Sciences, Vol. 6, No. 3, 2017, pp. 73-84.
[158] Interview with a woman farmer in Mtwara, August 2023.
[159] Interviews with local farmers in Mtwara, August 2023.

kwa wanaume. Kama alivyosema mwanamke aliyehojiwa, "serikali inajaribu kudhibiti harakati za watu, lakini huwezi kuzuia watu kuzuru familia zao[160]". Kauli hii inaonyesha jinsi gani mbinu kali pekee za kuweka usalama haziwezi kuhakikisha usalama, hasa kwa sababu udhibiti huu wa harakati za watu unaathiri uhuru na uendelezaji wa fursa za kiuchumi.

Katika masuala ya uchumi na mambo ya ndani, watu wanakuwa na wasiwasi zaidi katika kuitegemea serikali. Kuna kusuasua fulani katika kuwaamini wanasiasa hasa kutokana na dhana kwamba wanasiasa wamevunja ahadi zao. Jamii inaamini kuwa madhila yao hayajachukuliwa kwa uzito unaostahiki na viongozi wa kijamii na wangependa kuwa na nafasi zaidi ya kuwasilisha maoni yao kwa wawakilishi wao wa kisiasa[161]. Washiriki waliohojiwa katika utafiti huu wanaendelea kuamini kwamba Mtwara imepuuzwa kwa muda mrefu na serikali, na wangelishukuru kupata msaada zaidi wa serikali katika kutoa mikopo rahisi na mtaji wa kuanzisha biashara, katika kuingilia kati kwenye bei za soko[162]. Bei za mazao zimetajwa mara kadhaa kuwa ndio kadhia kubwa kwa jamii za eneo hili, kwani ni chanzo kikuu cha riziki katika sehemu ya kusini mwa Tanzania[163]. Zaidi ya hayo, kuna masikitiko makubwa kuhusiana na sekta ya gesi, ambayo ilitarajiwa kuongeza kasi ya maendeleo huko Mtwara, lakni uhalisia ukawa mdogo kuliko ilivyotarajiwa, na hivyo kusababisha chuki kubwa katika jamii[164].

Mwisho, asilimia 98% ya washiriki wa kike waliohojiwa katika utafiti huu, na 95% ya washiriki wa kiume wanaamini kuwa serikali ina jukumu la msingi linapokuja suala la kutatua mizozo kati ya jamii au makundi. Kwa ukweli, tayari ipo mifumo ya kutatua migogoro, kama vile kamati za ardhi katika ngazi ya kijiji au kata, vituo vya polisi, na watendaji kama mamlaka za mitaa na wazee ambao wanashughulikia mizozo wakati inapotokea[165]. Cha kuvutia ni kuwa, miongoni mwa waliohojiwa, wanawake wanaonekana kuegemeza wajibu mkubwa zaidi kwa serikali, huku asilimia 100% ya wanaume wakiamini ni jukumu la viongozi wa kidini kutatua mivutano hii.

## Asasi za kiraia

Takriban asilimia 82% ya wanawake walioshiriki utafiti huu, na asilimia 83% ya wanaume wanaamini kuwa asasi za kiraia (AZAKi) zina wajibu wa kutatua migogoro kati ya jamii au makundi. Wengi wa waliohojiwa wanaamini kuwa AZAKi ni muhimu katika kuongeza uelewa kuhusu amani pamoja na kujenga uwezo wa jamii wanazofanya kazi nazo. Aidha, AZAKi zinachukua jukumu kubwa katika

[160] Interview with a woman working in hair salon in Mtwara, August 2023.
[161] Interview with youth journalist in Mtwara, August 2023.
[162] In interviews with farmers, workers and civil society representatives in Mtwara, August 2023.
[163] Interview with farmer in Mtwara, August 2023.
[164] Interview with civil society representative in Mtwara, August 2023.
[165] Search for Common Ground, "Baseline and Conflict Assessment: Jenga amani Yetu", 2020.

kujenga nafasi salama za majadiliano ambapo wanaweza kuwaalika wadau husika ili kujenga jamii yenye amani zaidi na kupunguza migogoro, hivyo kuimarisha ushirikiano wa kijamii na kupunguza pengo kati ya jamii na wawakilishi wa taasisi. AZAKi zinaweza, kwa mfano, kuhakikisha ushiriki wa vijana katika maskani au kuchangia katika kuziunganisha jamii za ngazi ya chini na mamlaka za serikali au kati ya vikosi vya polisi na waendesha bodaboda.[166]. Kama mfano ulioelezwa na mwenyekiti wa kijiji: "Hapo kabla, wanajamii na polisi au jeshi hawakuwa wakishirikiana kwa urahisi, lakini sasa kwa msaada wa AZAKi, kila upande unazungumza na upande mwingine na kubadilishana taarifa kuhusu usalama[167]". Wawakilishi wa asasi za kiraia pia wanashiriki katika kutatua migogoro ya familia na ardhi. Kwa kufanya kazi na taasisi husika, AZAKi zinaweza pia kuhakikisha kuwepo kwa hali ya kubadilishana taarifa, kuongeza uelewa, kujenga uwezo na kushirikisha jamii.

Hata hivyo, kuna changamoto kadhaa ambazo zimebainishwa na waliohojiwa. Kwa mfano, shughuli nyingi za asasi za kiraia (CSO) zinatekelezwa katika mazingira ya mijini, kwa mujibu wa wahojiwa mbalimbali. Hii inaweza kuathiri vibaya ushirikishwaji, kwani jamii za vijijini mara nyingi ndizo zinazokabiliwa na ubaguzi zaidi na kutengwa. Mbali na hilo, juhudi za asasi za Kiraia zinategemea rasilimali zilizopo, ambazo mara nyingi huwa ni chache. Hali hii inaathiri huduma zinazotolewa na AZAKi au idadi ya watu au jamii zinazofikiwa.

Washiriki wametaja asasi kadhaa za kiraia. Miongoni mwao ni Shirika la Tanzania Building Future Organization (TABUFO), linalojikita katika mazungumzo ya amani yanayohusisha waendesha bodaboda na polisi, Shirika la Kimataifa la Search for Common Ground, ambalo linaandaa mafunzo kuhusu utatuzi na udhibiti wa migogoro, Mercy Corps na Might Society Against Poverty (MSOAPO).

## Vijana

Sehemu kubwa ya waliohojiwa wamesisitiza kwamba kundi linaloachwa mara nyingi katika mipango ya amani na michakato ya uamuzi ni watu wenye ulemavu (PWDs), wanawake na vijana. Wakati watu kutoka makundi haya wakialikwa katika shughuli, huchukuliwa kama wadau wadogo ambao wanaweza kuhusika katika kubadilishana maamuzi yaliyofanywa bila kuwashirikisha katika mchakato wenyewe wa kufanya maamuzi[168]. Ushiriki wa wanawake unakandamizwa zaidi na mila na desturi za kijamii. Kwa mujibu wa washiriki wa utafiti, kwa mfano, asilimia 53% ya wanawake na 65% ya wanaume wanaamini kwamba wanawake hawana fursa sawa za kushiriki katika jamii kama ilivyo kwa wanaume. Hisia hii inathibitishwa na watendaji wa serikali pia; kama mwakilishi mmoja alivyosema, "kutojumuishwa kwa wanawake lazima kutahusishwa na mfumo dume ambapo hata taasisi za kiraia zinatoa fursa zaidi kwa wanaume kuliko wanawake". Kuhusu watu wenye ulemavu,

[166] Interview with woman farmer in Mtwara, August 2023.
[167] Interview with community elder in Mtwara, August 2023.
[168] Interview with a young representative of civil society organisation in Mtwara, August 2023.

watu wengi wanaamini kwamba hawawezi kutoa mchango wowote chanya katika jamii na kwa hivyo huwaacha, bila kuwajumuisha katika jitihada yoyote ya maendeleo[169]. Hili ni kundi kubwa la watu, kwani kuna zaidi ya watu milioni 3.3 wanaoishi na ulemavu nchini Tanzania[170].

Kwa hakika kuna msukumo wa kijumla unaowavuta wazee wanaume kushiriki huku vijana na wanawake wakijizuia kushiriki katika kufanya maamuzi ya jamii. Kwenye hili, hali inafanana na ile ya Kenya; ambapo kuna mtazamo hasi kwa watu wazima wanaume wanaoamini kuwa ushiriki mdogo wa vijana, angalau kwa kiasi fulani unatokana na mtazamo wao wenyewe, au kama alivyosema mmoja wa watoa habari kuwa, "[vijana] wanachagua wenyewe kubaki nyuma[171]".

Maeneo haya ambayo yametoa uhuru wa ushiriki kwa kila mtu, kiuhalisia ni kwamba hayako jumuishi. Kwa mfano, mwandishi wa habari wa Redio ya Newala FM anasisitiza kwamba kama kijana si mwanachama wa tawi la vijana la chama tawala, taarifa muhimu zitampita bila yeye kujua[172]. Hata hivyo, mazingira ya kiuchumi ni magumu na yanakosa taarifa muhimu kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo kwa vijana[173].

Kwa muktadha huu, uchambuzi umeonesha baadhi ya mifano ya jitihada za kutambua uwezo wa vijana kama mabalozi wa mabadiliko chanya. Mfano mmoja ni ule wa klabu ya "Amani Yetu-Uhai Wetu[174]", the Global Peace Founation (GPF) ikishirikiana na TABUFO, ambayo inaonesha ujenzi wa amani makini kwa vijana wa Mtwara. Mwaka 2023, GPF pia ilishirikiana na Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO) kufundisha mashujaa wa amani na kuunda vilabu vya ujenzi wa amani.

---

[169] Interview with local government representative in Mtwara, August 2023.
[170] UN Women, "Strengthening the voice and agency of women with disabilities in Tanzania", January 2023.
[171] Interview with a woman farmer in Mtwara, August 2023.
[172] Interview with youth journalist in Mtwara, August 2023.
[173] UNDP, "#VijanaNaamani255: youth lead the charge toward safer societies in southern Tanzania", February 2023.
[174] McDonough R., "Engaging Tanzanian Youth in Peacebuilding Activities to Build Resilience and Prevent Violent Extremism", Global Peace Foundation, September 2023.

# TANGA

## Aina za migogoro na mifumo ya vurugu

Kwa upande wa Tanga pia aina kuu za vurugu ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa majumbani. Kama ilivyo kwa maeneo mengine, makundi ya wahalifu ya mitaani ni chanzo cha khofu kwa jamii za maeneo hayo.

Tanga ni lango muhimu la kimkakati la kuingilia Afrika Mashariki. Ikiwa katika eneo la mpaka, Tanga ipo katika hatari ya kuingiliwa na watu wenye msimamo mkali bila kugundulika[175]. Zaidi ya hayo, eneo hilo ni kituo cha kupitisha biashara haramu ya madawa ya kulevya kimataifa, wahamiaji haramu, na biashara ya binadamu[176]. Suala la uhalifu, hata hivyo, halioneshi kuwapa wasiwasi wakaazi wake. Asilimia 98% ya washiriki wa kike na 94% ya washiriki wa kiume wanasema wanajisikia salama kutembea katika maeneo yao, na ni asilimia 30% tu ya jinsia zote mbili wanachukulia matukio ya vurugu kama matukio yanayotokea mara kwa mara mkoani Tanga.

Aidha, ukatili wa kijinsia (kwa mujibu wa asilimia 43% ya wanawake na 45% ya wanaume ya waliohojiwa) na ukatili wa majumbani (kwa mujibu wa asilimia 33% ya wanawake na 45% ya wanaume waliohojiwa) umeelezwa kuwa ndio aina maarufu zaidi za ukatili. Machafuko ya kisiasa na ujambazi pia yametajwa, lakini na idadi ndogo ya washiriki. Katika muktadha huo, makundi ya kihalifu ya mitaani yanaonekana kuwa ni tatizo kubwa. Mfano unaotajwa sana ni kundi la Watoto wa Ibilisi, ambalo kwa kiasi kikubwa hufanya shughuli zao katika maeneo ya Magomeni, Mapinduzi, na Mikanjuni[177].

Shughuli za makundi ya kihalifu zinasababisha misuguano. Vyombo vya habari vya Tanzania vinaripoti kuwa serikali na wananchi wanalaumiana kuhusu vijana hawa wahalifu, ambapo wananchi wanaitaka serikali kusitisha ukatili wa makundi maovu, huku polisi ikiwalaumu wazazi kwa kutowafundisha watoto wao[178].

Kilichodhihirika ni kuwa, ukatili wa makundi unafungamana na matumizi mabaya ya pombe na dawa za kulevya, hasa heroini[179]. Heroini ni tatizo kubwa sana nchini Tanzania, kwa kuwa nchi hiyo ipo katika nafasi ya kupitishia au kuwa kituo cha dawa za heroin katika ukanda huu. Makadirio yanaonesha kuwa karibu nusu ya heroini inayoingizwa Afrika Mashariki inaishia Tanzania[180].

---

175 United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 14.
176 Ibid., p. 12.
177 Interview with *bodaboda* representative in Tanga, August 2023.
178 Burhani Y., Watoto wa ibilisi walivyoutikisa mji wa Tanga, Mwananchi, December 2022.
179 United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 12.
180 See, for example, reports from the Global Organized Crime Index for Tanzania.

Uwepo wa makundi ya kihalifu ya mitaani kunazidisha mtazamo hasi wa jamii dhidi ya vijana na kuongeza mivutano. Wengi waliohojiwa wamewaelezea vijana kama kundi linaloogoza linapokuja suala la uhalifu na vurugu huko Tanga, kwa sababu, kwa maneno yao, wengi wa wafuasi wa kundi hilo ni watoto wadogo. Sababu za kiuchumi zinazohusiana na umaskini, kuvunjika kwa familia, ukosefu wa makazi, matumizi ya dawa za kulevya, na ukosefu wa ajira zinadhaniwa kuwafanya vijana hawa, hasa wavulana, kuingia katika vurugu na shughuli haramu za usafirishaji, ikiwa ni pamoja na usafirishaji wa dawa za kulevya. Fursa ya kutengeneza pesa haraka na kwa urahisi[181] katika mazingira ya kutokuwepo kwa ajira ni jambo ambalo bila shaka linawafanya vijana kujiingiza katika shughuli za uhalifu.

Bado vijana wanachukuliwa kuwa ni watendaji wa vurugu, lakini wao huanza kufanya matendo hayo wakati wenyewe wakiwa kama ni waathirika. Lakini baadhi ya waliohojiwa wanakosoa sana vijana ambao wanajihusisha na tabia za uhalifu na kuwachukulia kama wasiotaka kufanya kazi[182]. Cha kushangaza ni kuwa kuwalaumu vijana kwa kuwa wazembe kunatokea katika mazingira ambayo fursa za ajira zipo, hii ikionesha uthabiti wa dhana hasi kama hizi.

Aina nyengine maarufu ya migogoro ni kuhusiana na ardhi, na kwa mujibu wa wahojiwa suala hili ni chanzo kikubwa cha kutoweka kwa usalama[183]. Mivutano kati ya wakulima na wafugaj iinajitokeza mara kwa mara na wakati mwengine hufikia kiwango cha vurugu. Visababishi vikuu vya migogoro hii ni pamoja na uharibifu wa mazao unaofanywa na mifugo, [udhibiti wa] makundi makubwa ya ng'ombe, na kukosekana kwa umakini wa serikali katika kusimamia migogoro hiyo pamoja na ufisadi[184]. Wahojiwa wanasisitiza kuwa watu wengi hawajui au hawafuati taratibu za upatikanaji na matumizi ya ardhi kama zilivyoelezwa katika Sheria za Ardhi[185].

Hali nyingine ya mvutano iliyojitokeza katika mahojiano na wadau inahusiana na waendesha bodaboda. Kama ilivyoelezwa na mwakilishi wa waendesha bodaboda, kundi hili linakabiliwa na changamoto za mara kwa mara na polisi ambao hutumia nguvu kubwa katika kesi za makosa ya kawaida ya barabarani. Mwakilishi huyo anaeleza kuwa kujenga uelewa na mazungumzo ya busara kati ya madereva na polisi ingekuwa ndio njia muafaka zaidi kuliko matumizi ya nguvu, faini au rushwa[186].

---

[181] Interview with community leader in Tanga, August 2023.
[182] Interview with street chairperson in Tanga, August 2023.
[183] United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 12.
[184] The Chanzo Initiative, "Clash Between Farmers, Pastoralists Leave Two Injured in Tanga", July 2022.
[185] Interview with religious leader in Tanga, August 2023.
[186] Interview with bodaboda representative in Tanga, August 2023.

Kuhusiana na suala la itikadi kali, Tanga siyo tu kitovu cha magendo kinachofadhili vikundi vya itikadi kali katika eneo hilo, lakini pia imekuwa ni eneo la mashambulizi kadhaa katika miaka ya hivi karibuni[187]. Hata hivyo, wahojiwa mara nyingi hawaitaji hali hiyo kama sababu kubwa ya ukosefu wa usalama mkoani Tanga (hii ni kwa mujibu wa asilimia 0% ya washiriki wa kike na asilimia 4% ya washiriki wa kiume). Mtazamo tofauti na huo unapatikana miongoni mwa wawakilishi wa vyombo vya usalama ambao wanauelezea ugaidi kama tishio kuu la usalama, ikifuatiwa na uhamiaji haramu, dawa za kulevya, migogoro ya ardhi, na migogoro ya kifamilia[188]. Hata hivyo, uwepo wa mitandao ya uhalifu wa kimataifa katika maeneo ya pwani ya Tanga unafanya iwe ngumu kwa jamii na polisi kuthibitisha ikiwa matukio ya vurugu yanayojitokeza ni ya kihalifu au yanahusiana na ugaidi, au ni mchanganyiko wa yote mawili[189].

## Viunganishi na vigawanishi

Dini na mikusanyiko ya kidini mara nyingi imeelezwa na wahojiwa kuwa ni kiunganishi kikuu cha jamii, na viongozi wa dini wameelezewa kuwa tayari kujitolea kwa utatuzi wa migogoro, hasa linapokuja suala la migogoro ya familia. Kwa mfano, mchungaji anayehudumia jamii kubwa Pangani anathibitisha kuwa: "Nasaidia katika kutatua migogoro ya kijamii ninapoombwa kufanya hivyo kwa msingi wa heshima yangu ya kidini katika wilaya[190]". Kwa hakika, dini inatambulisha njia ya maisha ya jamii ya watu wa Tanga kwa mujibu wa asilimia 100% ya washiriki wa kike na 92% ya washiriki wa kiume. Viongozi wa kidini, Tanga kama ilivyo kwa nchi nzima, wanafurahia kiwango kikubwa cha imani na heshima[191] na kwa maana hiyo wapo katika nafasi nzuri ya kuingilia kati migogoro ya jamii na familia, wakieleza maoni yao juu ya masuala nyeti.

Michezo nayo hutumika kama kiunganishi cha jamii, na mpira wa miguu hasa unaweza kuwaleta watu pamoja, hasa wanaume, bila kujali dini, kabila, au asili yao. Hii inaonekana, kwa mfano, katika kuunga mkono timu ya Coastal Union[192], klabu yenye makao yake mjini Tanga na inacheza Ligi Kuu ya Tanzania. Ushabiki wa mpira wa miguu hukithiri siku za mechi, huku mashabiki wakishiriki katika mazungumzo, mijadala, na matukio ya kijamii yanayozingatia michezo au mashindano na mechi za kirafiki ambazo hukuza udugu. Mkoani Tanga, mpira wa miguu unatumika kama jukwaa la mwingiliano wa kijamii, kuvunja vizuizi na kukuza uelewa kati ya makundi mbalimbali. Ushabiki wa pamoja wa mchezo huo unasababisha maelewano na kuruhusu watu kuungana na kushinda tofauti zao.

---

[187] Bofin P., "Tanzania and the Political Containment of Terror", Hudson Institute, January 2022.
[188] United States Institute of Peace (USIP), "Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania", March 2019, p. 13.
[189] Ibid.
[190] Interview with religious leader in Tanga, August 2023.
[191] World Faiths Development Dialogue (WFDD) , "Faith and Development in focus: Tanzania", September 2019, p. 1.
[192] Interview with *bodaboda* representative in Tanga, August 2023.

Kwa mujibu wa washiriki kadhaa, matukio ya kijamii mara nyingi huleta watu pamoja kama ilivyo kwa sherehe za harusi, mazishi na matukio mengine ya kitamaduni kama vile siku ya Maulid au sherehe za wavulana na wasichana (jando na unyago). Tabia jumuishi ya matukio haya, ambapo kila mtu hukaribishwa kwa ukarimu wa jadi wa jamii hizi, huzifanya kuwa na manufaa zaidi katika kuimarisha uhusiano wa jamii na kutengeneza fursa za mazungumzo na ushirikiano.

Pia, shughuli za kiuchumi na maslahi ya kibiashara hufikiriwa kuwa ni kiunganishi. Wakulima waliounganishwa na vikundi vya ushirika wa kilimo, jamii za wavuvi zinazoboresha mavuno yao, wajasiriamali wanaochochea ukuaji wa kiuchumi na manufaa ya pamoja ya ushirikiano katika kufuatilia malengo ya kiuchumi yanayofanana yapo dhahiri kwa watu wa Tanga. Mfano hai ni Jukwaa la Wadau Wasio wa Serikali katika Kilimo (ANSAF[193]) linalojikita katika ujumuishwaji wa kijamii, kiuchumi, na kisiasa katika matumizi endelevu ya ardhi. Kazi ya ANSAF inalenga kukuza ugawanaji sawa wa rasilimali, madaraka, na hasara miongoni mwa wadau muhimu katika sekta hiyo. Programu mbalimbali zinalenga kutoa fursa bora kwa wazalishaji wa vijijini kushiriki kikamilifu katika mazungumzo ya sera na maamuzi kwa ajili ya maisha salama.

Vivyo hivyo, mwanamke mfanyabiashara aliyehojiwa ametaja vikundi vya mikopo kwa wanawake, ambavyo vimejitokeza kama vyombo vyenye nguvu kwa uwezeshaji wa kiuchumi wa wanawake na maendeleo ya jamii[194]. Vikundi hivi kwa kawaida vinajumuisha wanawake wa eneo husika ambao wanakutana pamoja ili kukusanya rasilimali fedha, kuanzisha mfuko wa pamoja ambao wanachama wanaweza kukopa kwa ajili ya kuwekeza katika biashara ndogo au kushughulikia mahitaji yao binafsi ya kifedha. Hatua hizi siyo tu zinawapatia wanawake fursa za mitaji, lakini pia kutokana na kuwajibika kwao pamoja kifedha na kshirikiana katika ulipaji wa mikopo, kunasaidia ujasiriamali, ushirikiano na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla katika mkoa wa Tanga. Dini inatajwa kama kikwazo badala ya kuleta umoja. Tanga inakumbwa na migogoro mbalimbali ya ndani ya dini moja na kati ya dini moja na nyengine katika mazingira ambayo viongozi wa dini wana sauti kubwa na wanashiriki kikamilifu katika siasa[195]. Mazingira ya kidini ya Tanzania yana utata mkubwa, na mbali na mivutano kati ya Wakristo na Waislamu kwa mfano, ndani ya dini zenyewe kuna makundi yanayopingana kama vile Sunni na Shia, au kati ya Ansar al Sunna, wafuasi wakali na Waislamu wahafidhina, na wafuasi wa BAKWATA, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania ambalo ni mwakilishi rasmi wa serikali ya Tanzania kwa Waislamu. Hili la mwisho ndilo linalowatia wasiwasi zaidi wahojiwa. Migogoro hii inatokana na tafsiri tofauti za Uislamu, imani zake za kitaaluma na matendo, lakini pia inahusiana sana na harakati za ushawishi, uendeshaji wa misikiti na taasisi za kidini, na tafsiri ya sheria za Kiislamu.

---

[193] Cooperatives Europe, "Cooperatives and Peace: Strengthening Democracy, Participation and Trust", May 2019, 25 p. 76.
[194] Interview with woman entrepreneur in Tanga, August 2023.
[195] World Faiths Development Dialogue (WFDD) , Faith and Development in focus:Tanzania, September 2019, p. 11.

Wakati fursa za kiuchumi na biashara zikikutanisha watu pamoja, uhaba au kutokuwepo kwake kunaweza kuleta mgogoro katika mahusiano na kuchochea hasira ya watu wasiokuwa na fursa - na kwa sababu hiyo kuwa kigawanishi. Kama ilivyoelezwa na mzee mmoja, "Watu wengi Tanga wanapinga wale waliokuja tu katika eneo hilo na kujipatia fursa za ajira wakiwaacha wakaazi wa Tanga bila ya ajira[196]". Ukosefu wa ajira unaweza kuchochea chuki na ushindani, huku wakaazi wa eneo husika wakihisi kutishiwa na wageni wanaotazamwa kama wanyakuaji wa nafasi chache za ajira.

Mwisho, siasa na ukabila pia vimetajwa kama ni vigawanishi, hasa pale wanasiasa na wawakilishi wa serikali wanapochaguliwa au kutathminiwa kwa mujibu wa dini na makabila yao, na siyo kwa utendaji wao[197]. Hali hii inaleta changamoto katika taswira ya kisiasa, ambapo ufuasi wa mrengo fulani mara nyingi unachukua nafasi zaidi kuliko uwezo na ufanisi.

| VIUNGANISHI | VIGAWANISHI |
| --- | --- |
| Dini | Dini |
| Michezo hasa mpira wa miguu | Ukosefu wa fursa za ajira |
| Matukio ya kijamii na sherehe | Siasa na Uchochezi wa Kikabila |
| Shughuli za kiuchumi na maslahi ya biashara | |

## Uchambuzi wa wadau na uhusika wao

Zoezi la uchambuzi wa wadau lilifanyika kama sehemu ya uchambuzi wa migogoro ili kutambua wahusika wakuu katika migogoro na amani katika Mkoa wa Tanga. Sehemu hii inatoa maelezo ya kila moja kati ya makundi makuu yaliyotambuliwa, pamoja na taarifa zaidi zilizopatikana, kuhusu mitazamo na mazoea.

### Mamlaka ya serikali


Jumla ya asilimia 94% ya wanawake na 90% ya wanaume kati ya washiriki wa utafiti huu wanaamini kuwa ni jukumu la serikali kutatua migogoro kati ya makundi ya jamii. Washiriki wa mahojiano mara nyingi wanazungumzia kazi inayofanywa na serikali katika kuhakikisha usalama Tanga na wanatoa shukrani kwa ujumla kwa usalama uliofikiwa, pamoja na mipango ya polisi jamii iliyopo[198]. Kwa mfano, polisi jamii - ambayo ni neno la Kiswahili linalomaanisha watu wanaojitolea kutoka kijiji au mtaa kwa kutoa taarifa na kuwasaidia viongozi wa eneo husika na polisi kuhusu masuala ya usalama

[196] Interview with street chairperson in Tanga, August 2023.
[197] Interviews with a community leader and an entrepreneur in Tanga, August 2023.
[198] Interview with a small entrepreneur in Tanga, August 2023.

na ulinzi[199]. Kiujumla, watu wanajisikia salama zaidi kutokana na doria za usalama zinazoendeshwa na raia na wanadhani kuwa hatua hizi zinaimarisha ushirikiano na mazungumzo kati ya wanajamii na vyombo vya usalama[200]. Pamoja na hivyo, hata polisi jamii nayo imepoteza imani ya watu, kwani baadhi ya wahojiwa wameeleza kuwa baadhi ya polisi jamii wanatumia vibaya nafasi zao[201].

Mbali na kuweka hali ya usalama katika ngazi ya jamii, wahojiwa wamesisitiza kwamba serikali ina jukumu kubwa katika kutoa elimu kuhusu amani na usalama na kuandaa mikutano na serikali za mitaa kujadili masuala hayo. Mikusanyiko hii huthaminiwa sana kwa sababu husaidia kupunguza migogoro kwenye jamii kupitia mazungumzo ya busara na makubaliano ya pamoja[202]. Serikali za mitaa zinahusika katika kujibu changamoto zinazokabili vijana, kwa maoni ya asilimia 80% ya washiriki wanawake na 67% ya washiriki wa kiume waliohojiwa.

**Jadweli 5. Watu wanaosema kwamba serikali za mitaa zinashughulikia changamoto zinazowakabili vijana**




Kwa kuangalia suala la wanawake kipekee, wengi wa washiriki wa utafiti huu wanafikiri kuwa serikali za mitaa zinaweza kuboresha ustawi wa wanawake vijana. Kinachovutia zaidi ni kuwa washiriki wa kike wana mtazamo chanya zaidi (86%) kuliko washiriki wa kiume (59%). Hali ni tofauti linapokuja suala la wanawake kupata msaada kutoka taasisi za umma, ambapo washiriki wa kiume wengi wameonesha mtazamo chanya juu ya hilo kuliko wanawake (asilimia 77% kwa asilimia 65% mutawalia).

Maoni dhidi ya serikali yanakuwa hasi zaidi kuhusiana na mfumo wa haki ya jinai na uwezo wake wa kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia na kuhakikisha uwajibikaji[203]. Kuna kucheleweshwa katika

[199] United States Institute of Peace (USIP), “Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania”, March 2019, p. 16.
[200] Interviews with a religious leader and an entrepreneur in Tanga, August 2023.
[201] United States Institute of Peace (USIP), “Special Report: Violent Extremism and Community Policing in Tanzania”, March 2019, p. 16.
[202] Interview with an entrepreneur in Tanga, August 2023.
[203] Interview with a female entrepreneur in Tanga, August 2023.

kukamilisha kesi na kutoa hukumu, sheria zinazopingana kuhusiana na makosa ya ubakaji, na ukosefu wa rasilimali na ujuzi wa kushughulikia masuala kama hayo. Aidha, utamaduni wa kuripoti ukatili wa kijinsia kwa waathirika bado ni jambo la nadra sana na uwajibikaji pia upo kwa kiwango cha chini sana[204]. Pia, matatizo ya kiuchumi na ukosefu wa fursa za ajira yanapelekea mvutano na malalamiko mengi, hasa miongoni mwa vijana, dhidi ya serikali, ambayo inalaumiwa kwa kutokuwa na utayari wa kusaidia wakaazi wa Tanga. Kwa mfano, mmoja kati ya wahojiwa analalamika kuhusu jinsi serikali zilivyoiangusha jamii ya wazawa kwa kutowashirikisha katika ujenzi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (East African Crude Oil Pipeline (EACOP[205]) kati ya Uganda na Tanga, na pia kwa kutoajiri wafanyakazi wazawa katika mradi huo.

## Asasi za kiraia

Takriban asilimia 84% ya wanawake na asilimia 79% ya wanaume miongoni mwa washiriki wa utafiti huu wanaamini kwamba ni jukumu la asasi za kiraia kutatua migogoro katika jamii. Wote wanakubaliana kwamba Asasi za Kiraia zina athari chanya katika jamii na jukumu kubwa la kutekeleza hasa linapokuja suala la kuongeza uelewa na kujenga uhusiano wa amani. Asasi za Kiraia ni muhimu sana katika kuongeza uelewa kuhusu haki za binadamu, amani na umoja, hasa katika maeneo yaliyotengwa ambayo mara nyingi hayafikiwi na serikali kutokana na ukosefu wa rasilimali. Asasi za Kiraia pia zinaweza kujenga madaraja na kujenga nafasi salama ya mazungumzo yenye tija kati ya wadau tofauti, kwa mfano kati ya serikali za mitaa na wawakilishi wa serikali au vyombo vya polisi. Asasi za Kiraia, kwa mfano, ni moja kati ya wadau wachache ambao wanaonekana kujaribu kuamsha majadiliano kati ya dini moja na nyengine. Baadhi ya huduma zinazohusiana na ukatili wa kijinsia na matumizi ya dawa za kulevya pia hutolewa na Asasi za Kiraia. Kwa upande mwengine, AZAKi pia zinakabiliwa na changamoto na vizuizi kadhaa, hasa kutokana na rasilimali na uwezo mdogo na kwa uongozi wa kisiasa unaobadilika mara kwa mara, ambao unalazimisha mashirika kila wakati kubadilisha mipango yao ya maendeleo na uhamasishaji.

Taasisi ya kiraia iliyotajwa zaidi huko Tanga ni Tree of Hope Foundation, iliyoanzishwa mapema miaka ya 2000 kama Mradi wa Kudhibiti UKIMWI Tanga (Tanga Deanery HIV & AIDS Control Project), likifanya kazi katika wilaya tatu za Tanga, Pangani, na Mkinga juu ya kuwawezesha wanawake na vijana, kupambana na unyanyasaji wa kijinsia, na afya ya uzazi. Watu waliohojiwa pia wametaja UZIKWASA, shirika linalojitolea katika kuwawezesha jamii kwa maendeleo ya kujitegemea, haki za kijinsia, na uongozi unaozingatia mabadiliko; Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), mtandao wa mashirika kumi na mbili yanayojishughulisha

[204] Embassy of Ireland in Tanzania, "Addressing GBV and Gender Inequality Through the Tanzanian Criminal Justice System", October 2020.
[205] The East African Crude Oil Pipeline (EACOP), also known as the Uganda-Tanzania Crude Oil Pipeline (UTCOP), should be constructed by 2025 to transport crude oil from Uganda's Tilenga and Kingfisher oil fields to the Port of Tanga.

na watu wenye ulemavu; Shirika lisilo la kiserikali la kimataifa la MercyCorps; na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) ambalo tayari limetajwa.

## Vijana

Utafiti ulipotaka kujua ni makundi gani ambayo yametengwa, maoni tofauti yaliibuka kutokana na mazungumzo na waohojiwa. Mwakilishi wa serikali mwanamke alibainisha kwa mfano kwamba "wanaume wametengwa: hii ni kwa sababu hivi sasa kila kitu ni kuhusu uwezeshaji wa wanawake tu". Aidha, kiongozi wa kidini amesisitiza kwamba unyanyasaji wa kijinsia pia unaathiri sana wanaume vijana ambao wananyanyaswa na wanafamilia wa karibu[206]. Kwa mujibu wa mfanyabiashara, "Wazee mara zote wanatelekezwa kwa sababu baadhi wanaamini kuwa wao hawana chochote cha kuongeza katika jamii[207]". Ushuhuda mwingine umesisitiza umuhimu wa kushirikisha wavuvi wa kiume na wa kike katika mchakato wa kufanya maamuzi muhimu zaidi, kwani wanakabiliwa na shinikizo la mara kwa mara wanapokabiliana na wavuvi wa Kenya na vikosi vya Kenya katika maeneo ya mipaka[208].

Kwa Tanga, dhana ya kwamba wale wanaotengwa wametaka kuwa hivyo inawaathiri vikundi hivyo pia. Lakini, tofauti kubwa ni kwamba wengi miongoni mwao, hasa wale ambao hawana mahusiano na hawana wa kuwashika mkono, tayari wana wasiwasi na wanaamini kwamba hawatohusishwa kamwe. Hali ni ngumu zaidi kwa wanawake, ambao bado wanakabiliwa na vizuizi vingi vya kushiriki katika jamii inayowaona wanawake kama raia wa daraja la pili.[209].

Kuna mipango kadhaa iliyotekelezwa Tanga ambayo inashirikisha vijana katika kuzuia mizozo kwa njia shirikishhi ya kujenga amani. Miongoni mwa mifano hiyo kuna Chama cha Vijana Tanzania (TYC). TYC, iliyoanzishwa na vijana mwaka 2002, ni shirika mwamvuli linalojikita katika kuwawezesha vijana. Kwa sasa shirika hili linajumuisha zaidi ya AZAKi 120 za vijana na Mashirika ya Kijamii (CBOs), Vikundi vya Ujasiriamali vya Vijana (YEG) 249, na mamia ya vijana mmoja mmoja kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Mfano mwingine ni taasisi ya Youth Peace Maker (YPM) Tanzania, yenye makao yake Tanga, ambayo inajishughulisha na utoaji wa elimu, ujuzi na kuwawezesha vijana, wanawake na jamii kwa ujumla.

[206] Interview with a religious leader in Tanga, August 2023.
[207] Interview with an entrepreneur in Tanga, August 2023.
[208] Interview with an entrepreneur in Tanga, August 2023.
[209] Ramadhani I., "How Pangani villagers push for gender and climate justice", The Citizen, March 2023.

## NAFASI YA UTAMADUNI WA WASWAHILI NCHINI TANZANIA

Kwa mujibu wa utafiti, utamaduni wa waswahili unelezea njia ya maisha ya jamii za waswahili kwa mujibu wa maelezo ya asilimia 85% ya washiriki wa kike na 86% ya washiriki wa kiume waliohojiwa Mtwara. Kwa upande wa Tanga, washiriki wanaamini kuwa dini ni muhimu zaidi katika kueleza maisha ya jamii (asilimia 100 ya wanawake na 92% ya wanaume) kuliko utamaduni wa Kiswahili (asilimia 88 ya wanawake na 81% ya wanaume). Kwa ujumla, Uislamu unafikiriwa kuwa una uhusiano wa karibu na utamaduni wa Kiswahili, ukiwakilisha moja ya nguzo zake muhimu.

Kwa kuchambua majibu ya wazi ya washiriki wa utafiti, utamaduni wa Waswahili unaathiri mila, tabia, na matendo yanayounda maisha ya watu wanaoishi Tanga na Mtwara. Lugha ya Kiswahili kwa hakika ina nafasi muhimu katika utambulisho wa jamii hizi. Ni lugha inayounganisha jamii za makabila tofauti na kuimarisha hisia ya kujisikia sehemu ya jamii hii. Kubadilishana taarifa kwa njia ya mdomo ni njia muhimu ya kusambaza na kupata habari zinazohusu usalama. Mtandao ulioshikana wa mahusiano ya watu unatoa fursa ya kusambaza taarifa muhimu kwa haraka huku ikiimarisha hisia ya pamoja juu ya usalama. Mbinu hii ya mawasiliano ya ngazi ya chini sio tu inaimarisha uhusiano wa jamii na kuongeza nguvu ya jamii, lakini pia inathibitisha umuhimu wa maarifa ya kienyeji katika kukabiliana na changamoto za usalama. Zaidi ya lugha, utamaduni wa Kiswahili unajumuisha, kama ilivyo kwa Kenya, mitindo ya mavazi, vyakula vya jadi, na mila. Washiriki wa utafiti kutoka Mtwara na Tanga wanauona utamaduni wa waswahili kama wenye ukarimu, lakini pia unaopenda kusema sana na kupendelea kusambaza habari za uvumi. Njia ya mashirikiano katika maisha inaonekana katika matukio mbalimbali yaliyotajwa na washiriki, kutoka sherehe za jadi hadi shughuli za kiuchumi kama uvuvi na ukulima wa mwani. Utamaduni huu pia unaonekana kuruhusu mabadiliko, ukiendana na mabadiliko kila baada ya muda.

Hata hivyo, kuna changamoto zilizobainishwa. Baadhi ya washiriki wa utafiti kutoka Tanga na Mtwara wanaeleza wasiwasi wao, katika maswali ya wazi, kuhusiana na uadui, majungu, na matusi ndani ya jamii, wakati wengine wakizungumzia uvivu na uhafidhina. Aidha, kutokana na athari ya teknolojia, kuna mgongano wa wazi kati ya ukale na usasa. Washiriki wa utafiti wameonesha wasiwasi juu ya kuharibika kwa taratibu na desturi za kitamaduni, huku wengine wakiuona utamaduni kuwa hauko imara au unoathiriwa na vitu kutoka nje. Licha ya hivyo, kuna hisia kubwa ya ufakhari na umoja, na Waswahili wanathamini maisha ya umoja, kusaidiana, na kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Jumla ya asilimia 91% ya washiriki wa kike na asilimia 98% ya washiriki wa kiume huko Mtwara wanaamini kuwa utamaduni wa Waswahili unapaswa kuendelezwa, ambapo mawazo hayo kwa upande wa Tanga ni asilimia 96% ya wanawake na asilimia 94% ya wanaume. Ingawa, wengi wa

washiriki kutoka Mtwara, hasa wanawake, hawaoni kwamba utamaduni wa Waswahili unakuza usawa wa kijinsia (asilimia 38% ya wanawake na asilimia 55% ya wanaume), wakati Tanga asilimia 53% ya wanawake na asilimia 45% ya wanaume wanaamini hivyo.

Washiriki wa utafiti wanaeleza sababu kadhaa kwa nini utamaduni wa Waswahili unachangia katika amani. Moja ya sababu hizo ni mtangamano wa mila za kitamaduni za Waswahili, ambazo huchochea hisia ya umoja kati ya wanajamii. Ngoma na muziki wa asili huambatana na mikusanyiko ya kijamii kama vile ndoa, mazishi na mila za kuingia utu uzima (jando na unyago), ambazo huchukuliwa kama ni nafasi nzuri ya kuamiliana katika mazungumzo. Matukio haya siyo tu ni viunganishi, bali pia huchochea ushirikiano na mazungumzo ya jamii, huku yakiimarisha mahusiano ya kijamii. Utamaduni wa Waswahili unachukuliwa kama ni chombo cha kuimarisha uhimilivu wa kijamii. Kwa maoni ya washiriki wa utafiti, utamaduni wa kusaidiana wakati wa nyakati ngumu, unachangia kutendeana wema katika jamii na kuheshimu haki za binadamu. Kitu kingine cha kuvutia ni ukweli kwamba mila na desturi za kitamaduni zinazohusiana na sherehe huendeleza maadili kwa vijana. Hii si tu elimu kwa kizazi kipya bali pia inaimarisha mahusiano kati ya vizazi.

# MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO

Kutokana na mifano iliyoelezwa hapo juu, mapendekezo yafuatayo yanatolewa ili kuongoza utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa amani chini ya mradi wa Kujenga amani, na hata baada ya mradi:

1. **Kushirikisha makundi muhimu ya vijana ikiwa ni pamoja na wale waliotengwa.** Changamoto kubwa inayokabili mazingira yaliyochambuliwa katika utafiti huu ni umaskini, kutengwa, na ukosefu wa fursa. Hivyo kuna haja ya kukuza ushirikiano katika ngazi zote, na kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma, hasa wale wanaohusiana, kwa namna moja au nyingine, na migogoro. Kuwatafuta na kuwashirikisha vijana walioachwa nyuma ambao wanaathiriwa zaidi na suala hilo ni muhimu ili kufikia matokeo endelevu. Wahusika wa mradi wanapaswa kuyajumuisha makundi muhimu zaidi ya vijana yanayojihusisha na vurugu, yaani wafuasi au waliokuwa wafuasi wa makundi ya kihalifu, na vijana walio katika hatari ya kujiingiza katika makundi hayo, kama wale wanaotumia dawa za kulevya, vijana wanahudhuria shule pamoja na vijana walioacha shule, na vijana wasio na ajira. Aidha, kwa kuwa miradi mingi inalenga maeneo ya mijini, hatua maalum lazima zichukuliwe kuzishirikisha jamii zinazoishi maeneo ya vijijini, ambazo mara nyingi husahauliwa na miradi ya maendeleo na hivyo kukosa sauti.

2. **Kushirikisha wadau muhimu hasa taasisi, wazee na viongozi wa kidini.** Wadau wanaoaminika na kuheshimika wanapaswa kuhusishwa katika hatua zote za mradi, kuanzia tathmini ya mahitaji ya jamii hadi utekelezaji wa shughuli za mradi. Wadau hawa ni pamoja na wawakilishi wa serikali za mitaa pamoja na wazee na viongozi wa kidini wa jamii. Pia, kuna haja ya kuwatambua mashujaa miongoni mwa wawakilishi wa serikali na wadau wa jamii. Hii bila shaka itarahisisha utekelezaji wa mradi kwa kuweka bayana nafasi ya kila mdau jinsi wanavyoweza kusaidia utekelezaji wa mradi ipasavyo.

3. **Kushirikisha polisi na maafisa wa usalama katika mazungumzo na vijana.** Jambo jengine ambalo ni muhimu kulifanyia kazi ni ushirikishwaji wa polisi: Imani zaidi kati ya polisi na vijana inahitajika ili kukabiliana na changamoto za usalama wa ndani. Unyanyasaji wa polisi kwa hakika ni wasiwasi mkubwa kwa vijana. Mazungumzo kati ya vijana na polisi kuhusu masuala ya amani na usalama yanapaswa kuandaliwa ili kuondoa hofu kuhusu jeshi la polisi machoni mwa vijana.

4. **Kuhakikisha umiliki wa jamii.** Ni muhimu kuihusisha jamii inayolengwa kutoka mwanzo ili iweze kuwa na ufahamu wa mada na kujisikia ina umiliki wa programu. Ni muhimu kuwahimiza kutoa maoni yao kipindi chote cha utekelezaji wa mradi, katika mchakato wa mashauriano ya wazi. Mradi unapaswa kusisitiza kwamba amani na usalama ni jukumu la kila mmoja. Mpango huo

unapaswa kukubali mabadiliko, kutoa majibu kwa mahitaji ya jamii, na kuweza kubadilika kwa haraka kadiri ya hali itakavyobadilika.

5. **Kutumia fursa na mifumo ya sera iliyopo.** Mradi pia unapaswa kutumia vyema miundo ya mazungumzo iliyopo na michakato ya upatanishi. Kwa mfano, ni muhimu kushirikisha Mpango Kazi wa Kwale (CAP) kuhusiana na Mpango wa Kushirikisha wanawake kwenye Usalama (WPS). Mradi pia unapaswa kuwa na lengo la kushirikiana na miradi mingine ya kijamii ili kutengeneza jitihada za pamoja na zenye mshikamano za zaidi kusaidia vijana na jamii kwa ujumla. Pia, kuna haja ya kuoanisha shughuli za mradi na nyaraka, sera, miundo na mazoea yaliyopo ili kupata kukubalika.

6. **Kujikita katika kujenga na kukuza ushirikiano katika maeneo salama.** Ni muhimu kwa mradi uweze kushirikisha watu wa makundi tofauti kwa njia shirikishi na salama. Baadhi ya wakati, kuna haja ya kuandaa shughuli maalum kwa makundi maalum, kama vile kjinsia au kuandaa mikusanyiko iliyolenga wazee au dini maalum, lakini kwa ujumla makundi yote yanayohusika ni lazima yashirikishwe kwa usalama na kwa umakini.

7. **Kujenga uwezo katika mazingira ya amani na usalama.** Katika baadhi ya kesi, vijana wanakosa uwezo na utaalamu wa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa amani na usalama. Ni muhimu sana kujenga ufahamu zaidi pamoja na maarifa na ujuzi. Watu wanapopatiwa habari, hushiriki. Aidha, vijana wanaweza kujengewa uwezo wa kuelemisha na kupatanisha katika masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na migogoro ya ardhi. Ujuzi huu ni muhimu kwa watu wale ambao, kutokana na kazi zao au kwa imani wanayopewa, wanaalikwa kila siku kusimamia na kutatua migogoro ya kijamii na familia.

8. **Kukuza uelewa na mazungumzo kati ya vizazi.** Inapaswa kuwepo maelewano mazuri kati ya wazee na vijana na kuwepo nafasi ya mazungumzo miongoni mwa rika tofauti. Serikali za mitaa pamja na wazee wanahitaji kuongeza ufahamu wao juu ya vipengele vya kisaikolojia vinavyoweza kusaidia kuwaelewa na kuwasaidia vijana. Kuhusiana na hili, kuna haja pia ya kusaidia wazazi, hasa wale ambao ni vijana sana na wasio na ufahamu, kujenga mahusiano yenye nguvu na yenye afya na watoto wao.

9. **Kusaidia ushirikishwaji wa vijana.** Vijana wanahitaji kushirikishwa katika mazungumzo na jitihada za amani na usalama. Wanapaswa kuwa na nafasi salama ya kutoa maoni na michango yao. Uwezo wao wa kujenga amani na upatanishi wa migogoro unapaswa kuimarishwa ili waweze kutumia uwezo huo katika maisha yao ya kila siku, hivyo kuonesha uwezo wa vijana kwa mabadiliko ya kimatendo. Wadau wanapaswa kushirikishwa katika kuendeleza fursa zaidi kwa vijana.

10. **Kukabiliana na pengo la la kuwarudisha vijana katika njia sahihi ya jamii.** Mara nyingi, kuna ukosefu wa msaada kwa vijana wanaotoka katika makundi ya uhalifu na vikundi vya wanamgambo ambao baada ya kutoka huko hushindwa kupata ajira na kukubalika katika jamii. Ni muhimu kuwasaidia wafuasi vijana wa makundi hayo kurudi katika jamii.

11. **Kutumia njia ya elimu rika.** NI muhimu kwashirikisha vijana katika kuwaelimisha wenzao kuhusu masuala kama ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya au tabia zisizo nzuri kwa jamii. Mashujaa hawa vijana wanapaswa kushirikisha wenzao na kuelewa matatizo yao ili kwa pamoja waweze kutafuta suluhisho.

12. **Kuepusha matumizi mabaya ya dawa kwa vijana.** Kuna uhusiano wa karibu kati ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya na uhalifu. Watumiaji wa dawa mara nyingi hufanya uhalifu ili kupata fedha za kulipia madawa. Zaidi ya hayo, wahalifu wengi mara nyingi huwa wanaendeshwa na nguvu ya madawa pale wanapotekeleza uhalifu. Kutokuwa na ufahamu miongoni mwa vijana kuhusu madhara ya matumizi mabaya ya dawa inatajwa kama moja ya sababu kuu za vijana kujihusisha na tabia hii mbaya.

13. **Kuwa makini na hali tete ya migogoro**. Wakati wa kuchagua washiriki na jamii za kufanya kazi nazo katika miradi, ni muhimu kuepuka kuchochea mivutano. Kwa kuwa mara nyingi fedha za maendeleo na fursa zimekua zikizua migogoro na hata machafuko kutokana na jamii zilizotengwa, ni muhimu sana kuwa makini wakati wa kuchagua kata na vijiji vinavyolengwa na miradi. Maamuzi yanapaswa kufanywa kwa njia shirikishi kwa kufuata utaratibu wa kuanzia chini kwenda juu.

AGENCY FOR PEACEBUILDING

www.peaceagency.org